# *Lakini Haikuwa Hivyo Tangu Mwanzo*

Kwa hiyo, ni kama tu mtu aliye na pesa kwenye benki, bali hajui jinsi ya kuandika hundi, na huyo mwingine anaweza kuandika hundi, wala hana pesa kwenye benki, kama ungeweza kuwaleta hao wawili pamoja, ungezipata.

2 Laiti Wapentekoste wangeweza tu kutambua ya kwamba wao si takataka ya dunia, wao ni wana na binti za Mungu, warithi wa vitu vyote kupitia Kristo! Lakini mradi Shetani anaweza kuwafanya mwogope kudai urithi wenu, basi amewanasa, unaona, mradi mnauogopa. Msiogope Neno lolote ambalo Mungu aliandika, shikilia tu *fungu* lako kwenye kiakifishi chochote kilichoko Humo ndani kwa sababu ni cha ukweli, ni cha kweli kabisa. Halafu basi songa mbele tu, kama huwezi kuona unakoelekea, mradi tu unafuata Neno, songa kwa vyovyote vile.

3 Kama vile Ibrahimu, yeye hakufanya hivyo, hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini, alikuwa na nguvu wakati wote, akimsifu Mungu, akijua itatendeka kwa vyovyote vile. Mnaona? Nasi ni watoto wa Ibrahimu. Bwana akipenda, hilo ndilo ninalotaka kuwazungumzia Jumapili alasiri: *Ibrahimu Na Uzao Wake Baada Yake*. Nasi tunatarajia kuwa na ibada kuu ya uponyaji Jumapili alasiri.

4 Nafikiri ni zuri sana, ni ombi langu daima, ya kwamba wakati kuna makanisa mengi yanayodhamini, hebu tusiwe na ibada ya Jumapili usiku tusije tukawaondoa ndugu zetu, watu wetu kutoka makanisani mwao na kadhalika. Nafikiri kila mtu unapaswa kuwa kwenye wajibu wako wakati kanisa lako limefunguliwa. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli kabisa. Unapaswa kusimama pamoja na mchungaji wako, na kusimama pamoja na halmashauri yako, na kusimama pamoja na kanisa lako, na, lakini wakati tunapokuwa na mkutano wa mwungano kama huu, kama tunaweza kuufanya Jumapili alasiri, basi kila mtu anaweza kurudi kanisani mwao labda amechochewa na jambo fulani alilosema mtu fulani, ama ushuhuda, ama jambo fulani alilofanya Bwana, ama wimbo, ama mahubiri, ama kitu fulani. Na—nami nafikiri basi tunaweza kuendelea tu kusonga mbele namna hiyo.

5 Na mimi, kwa ajili ya pesa, sijawahi ku-. . .Nina umri wa miaka hamsini na miwili hivi majuzi, nami nimekuwa katika huduma, katika karibu miaka thelathini na mmoja, kamwe sikuchukua sadaka maishani mwangu, kamwe sijachukua

sadaka moja maishani mwangu, wala sikusudii kuchukua. Kwa hiyo, nilikuwa nikifanya kazi, nilihudumia Maskani ya Kibaptisti huko Jeffersonville kwa miaka kumi na saba bila hata senti moja, nilifanya kazi kama mlinzi wa wanyama nchini, nyaya za umeme, chochote ningepata cha kufanya, na kujigharamia mwenyewe, na kusaidia kulijenga kanisa. Nami siamini ya kwamba—ya kwamba. . .Siko kwenye mpango huu mkubwa wa pesa.

6 Na vipi kama ilinibidi kupata pesa nyingi kadiri inavyowabidi baadhi ya hawa ndugu kuwa nazo? Vipi kama ilinibidi kulipia matumizi ya Billy Graham? Vipi kama ilinibidi kulipia matumizi ya Oral Roberts? Kamwe nisingeweza kuja mahali padogo kama hapa na kufanya mkutano. Lakini ninapenda kujiweka mahali ambapo sina gharama ya matumizi, ndipo basi popote Bwana aniongozapo naweza kwenda, mnaona, siko cini ya masharti yoyote.

7 Nilifanya tu uamsho katika kanisa la watu ishirini. Kulikuwa—kulikuwa kubaya sana, bali tuliufanya, naye Bwana akabariki na kufanya jambo kubwa. Watu walisimama katika hali ya hewa sufuri, wakilia na kuhema, na pumzi ikagandia usoni mwao, bali waliokoka. Kwa hiyo kuna tofauti gani, mradi tu wanaokolewa?

8 Wala sina pesa zozote, nadhani ninii yangu, kama ningeangalia akaunti yangu usiku wa leo, nayo ilikuwa. . . kama mimi sijaishiwa kabisa, siwezi kuwa na zaidi, angalau, dola mia moja na hamsini. Kwa hiyo ningefanyaje na hizo ambapo, labda, inambidi Bw. Roberts kutumia karibu dola elfu saba, ama nane, kumi kwa siku? Loo, nisingekuwa na hizo hata iweje. Jamani, loo, jamani! Mungu alijua vema kuliko hilo, alijua sina, sina bongo la kutosha kushughulikia mambo kama hayo. Uh-huh. Ka—kamwe nisingeweza kufanya hivyo. Ninashukuru sana kwamba Mungu anao watu ambao Yeye. . . kufanya hayo.

9 Niliposimama si muda mrefu uliopita, Ndugu Oral Roberts, ninakumbuka wakati alipokuwa na mkutano wake wa kwanza, alihudhuria mkutano wangu hapa St. Louis, na, ama, Jiji la Kansas, hema dogo lililochakaa limepigwa ng'ambo ya pili, naye akasema, "Ndugu Branham, unafikiri Mungu atasikia maombi yangu kwa ajili ya wagonjwa?"

Nikasema, "Atasikia maombi ya *mtu yeyote*, Ndugu Roberts."

10 Pia ninamkumbuka Tommy Osborn, wakati alipojisulubisha mwenyewe usiku ule wakati yule mwenye pepo alipokimbia jukwaani kuniua, mmesoma hadithi yake, Portland Oregon, ndipo akaja nyumbani kwangu, akasema, "Ndugu Branham, loo, unafikiri nina karama ya uponyaji?"

11 Nikasema, “Ndugu Osborn, wewe ni kijana mwanamume shupavu.” Nikasema, “Kama hili likiendelea litakuwa kama uamsho mwingine wowote, itakuja kutokea kwamba jamaa hataona kwamba ana huduma isipokuwa awe na ibada ya uponyaji.” Nikasema, “Usiwazie hilo.” Nikasema, “Kama Mungu alikuita kuhubiri Injili, Yeye alikuita kuwaombea wagonjwa.” Nami nikasema, “Dumu tu moja kwa moja nalo.” Unaona?

12 Wachungaji wenu wana haki zile zile za kuwaombea kama mwinjilisti yeyote hudumani. Na kama mchungaji wako hayuko, jirani yako mwema aliyeokolewa na Mungu anaweza kufanya vivyo hivyo, mume wako, ama ndugu yako, mtoto wako, ama yeyote yule. “Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa.” Hiyo ni kweli.

13 Kwa hiyo kamwe sijaribu kupata pesa. Basi hao ndugu wawili niliowataja, watu wawili wema, waaminifu, wazuri, waliookolewa na Mungu, ni T. L. Osborn na Oral Roberts. Hiyo ni kweli kabisa, wao ni watu wazuri. Ninawajua wote wawili tangu huduma yao ilipoanza, nao ni ndugu wazuri sana.

14 Nami nilienda kwa Ndugu Osborn hivi majuzi, na kule wakati nilipokuwa na mkutano huko Tulsa, nami nikaangalia jinsi Mungu alivyokuwa amembariki. Naye ni mmishenari mashuhuri, hufanya kazi ya umishenari. Na pesa mnazomtumia Ndugu Osborn hakika zinatumika vizuri, yeye ni mtu mzuri, aliyeokolewa na Mungu. Basi nikaingia kwake, akanikumbatia, akaanza kulia, akanionyesha mahali pote ambapo alishakuwa, akasema, “Ndugu Branham, hiyo ni sehemu ya huduma yako.” Akasema, “Kama usingalienda na kufanya kama Bwana alivyofanya, na—na kwa . . . alivyokwambia ufanye . . . ” kasema, “Mimi ni mmojawapo tu wa wanafunzi wako,” tuseme. Wazieni, mtu wa hadhi hiyo akimwambia mtu duni kama mimi kwamba alikuwa ni mwanafunzi wangu, hiyo inahitaji roho tamu sana, nyenyekevu.

15 Halafu basi, nilipokuwa kule, Ndugu Oral Roberts alianguka na kujeruhi mguu wake. Nami nikaingia kwenye nyumba yake kubwa ya kupendeza kule, wala nisingalitendewa mema zaidi kama ningalikuwa Malaika aliyetoka Mbinguni, nilipoenda kumwombea. Naye alikuwa na goti ambalo lilikuwa . . . loo, lilikuwa katika hali mbaya sana. Basi nilipokuwa nikiomba, mishipa ya damu ilishuka na kufanya *V* kubwa juu ya goti lake, akasimama moja kwa moja na kuondoka.

16 Kwa hiyo nikaenda katika maboma yake, na ni nyumba kubwa, nzuri, ya kupendeza jinsi gani, nikalia tu. Nilipotoka nje na kuliangalia jengo lake kubwa mno pale, jinsi lilivyojengwa vizuri, kila kitu katika umbo la utatu, kisha nikaona kile kioo pale cha mikono ikishuka chini, halafu nilipotoka nje na kuangalia, sijawahi kuona chochote popote ulimwenguni kama

hicho popote, nami nikawazia, "Ee Mungu, Yehova Mkuu, jinsi ninavyoshukuru! Hiyo inaonyesha imani ya mtu mmoja ambaye kweli anaweza kumshika Mungu, na kufanya kitu kama hicho. Jinsi ninavyoshukuru!"

17 Ndipo Shetani akaniambia, akasema, "Yeye hakujali sana. Vipi kama akija kwako na kuona taipureta moja ndogo imewekwa pale mwishoni mwa trela? Hiyo ingekuwa ofisi ya aina gani?"

18 Nikasema, "Vema, ninafanya vizuri niwezavyo, hivyo tu." Nina wakati mgumu wa kujibu kila barua. Ndipo nikaangalia juu, nikawazia, "Jamani, hakika ningechukia hao ndugu kuja nyumbani kwangu, na kuona ofisi yangu." Basi nilikuwa tu nimesimama pale, jambo fulani tamu likatukia, nami kamwe sitalisahau, dhahiri tu kama nilivyopata kusikia sauti maishani mwangu, Yeye akasema, "Lakini mimi ndiye Sehemu yako."

19 Nami nikasema, "Asante, Bwana. kwa furaha nitapitia njia hiyo, maana siwezi kupata akili za kuiendesha redio ya ulimwenguni kote kama Ndugu Roberts, na maelfu ya watu anaowafikia. Lakini katika njia yangu ndogo, nyenyekevu, kama utanisaidia tu, na uwe Sehemu yangu, basi nitakufuata tu, na popote utakaponiongoza basi ni—nitafanya katika hiyo njia ndogo, jinsi. . . " Maana hatuna budi kuwa na mawe madogo, kwa namna fulani yanaingiana na mawe makubwa.

20 Ninayo saa ya mkono hapa ambayo walinipa huko Uswisi, nayo ina mizunguko mingi midogo, chungu nzima, zote si springi kuu, lakini inabidi zote zifanye kazi kufanya . . . kutunza wakati. Kwa hiyo hivyo ndivyo ninavyowazia, sote pamoja hufanya, sote tunapitia njia zetu ndogo kutunza wakati, hasa kabisa.

21 Na hiki *hapa* kidole changu, hakika si bongo langu, hakika si jicho langu, wala sikio langu, lakini natumaini kamwe hakiamui kutokuwa kidole, kwa sababu ati si jicho langu, wala sikio, kwa kuwa mimi . . . itakuwa ni vigumu kufanya kazi bila hicho.

22 Na labda kanisa lenu dogo, mnasema, "Vema, Ndugu Branham, sisi ni kundi dogo tu la watu." Hilo halijalishi, unatimiza sehemu fulani katika Mwili wa Kristo, kwa hiyo nenda tu, songa mbele tu jinsi Roho Mtakatifu anavyokuongoza. Zawadi yako itakuwa vivyo hivyo mwisho wa siku.

23 Loo, Yeye si anapendeza? Sasa, katika siku moja ama mbili usiku, Bwana akipenda, tunataka kuanzisha ibada zetu za uponyaji, tukiendelea kwa Roho Mtakatifu na kuangalia yale afanyayo. Sasa, watu wengi watauliza maswali, hasa wakati hawa wavulana watakapoanza kusambaza picha hizi za Nguzo ya Moto, na kutakuwako na maswali ya kila namna. Kwa hiyo ninatumaini ya kwamba kwenye ibada za alasiri, na kadhalika, kwamba wanawafundisha kwamba hiyo ni nini, mnaona, hasa.

24 Ni wangapi wamewahi kuiona hiyo picha? Nakisia karibu sisi sote tumeiona. Imekuwako kote ulimwenguni. Kama . . .

Hii hapa, tuliyo nayo sasa, ilipigwa huku Houston, Texas, na ikachunguzwa na FBI, hiyo iko kwenye alama ya vidole na hati, ambayo ni George J. Lacy.

25 Naye aliniambia siku hiyo, nikisimama pale kwenye jengo la Shell ambapo magazeti yao yote, na kadhalika yalikuwa, alisema, "Bw. Branham, nimekuwa mmojawapo wa wakosoaji wako." Akasema, "Daima nimesema ya kwamba ilikuwa ni saikolojia, ulikuwa ukisoma mawazo ya watu, na hao watu waliosema wameona Nuru, na kadhalika," kasema, "nilisema hiyo ilikuwa ni saikolojia tupu kwa sababu waliibuni." Lakini kasema, "Kasisi Branham, jicho la kimitambo la kamera hii halitapiga picha saikolojia, Nuru iliigusa lenzi." Akasema, "Ilikuwapo."

26 Kwa hiyo kama mtu yeyote akiwauliza, ninawapa maoni yangu manyenyekevu, kama Unyakuo ungekuja usiku wa leo, nasi tungeenda ilivyopangwa, sisemi hili ati niwe mnyenyekevu, ninalisema kwa sababu linatoka moyoni mwangu, maana kama mtu akinena kutoka kinywani mwake kitu ambacho hakiko moyoni mwake, basi yeye ni mnafiki, naye ni mbaya kuliko kafiri, lakini kama Unyakuo ungekuja, ninyi nyote, labda, mngenitangulia, hiyo ni kweli.

27 Lakini ninashukuru sana kujua ya kwamba Mungu, bila elimu, bila uwezo wowote, bali kwa karama nyenyekevu, Mungu amenijalia kumletea watu milioni moja, ama mbili, jinsi, vizuri nipaswavyo kufanya. Wala sina ninii . . . Nilitoka, nikasalimisha tu ushirika wangu kutoka kwene, si ushirika, bali kadi ya ushirika kutoka kwa kanisa la Kibaptisti, Baptisti ya Kimishenari, kusudi niwe na ushirika na Wapentekoste, na pamoja na watu wote, Methodisti, Baptisti, Presbiteri.

28 Nami nimeninii . . . Nilikuwa na mwaliko wa kujiunga na—na Assemblies of God, Church of God, na—na Pe—Pentecostal Holliness, na la Umoja, na U—U—United Pentecostals, na makundi yote mbalimbali, ambayo yote ni watu wazuri, nionavyo mimi, kuna Wakristo katika hayo yote. Lakini nimejaribu kusimama kwenye pengo kati yao wote, na kusema, "Sisi ni ndugu, hebu . . . " Na ushawishi wowote mdogo nilio nao kwa Injili, ambao Mungu amenipa, kamwe sijaribu kuuweka kwenye madhehebu yoyote, bali juu ya Kristo, ili kwamba wote wapate kumwona na kumwamini.

29 Sasa, ile, Nuru ile, hebu niiendee kwa muda kidogo tu maana mara nyingi . . . Ilipigwa huko Ujerumani hivi majuzi. Waliuliza kama kamera zao . . . Nayo Ujerumani ina *lenzi* hodari, sote tunajua hilo. Nami nilikuwa kwenye kiamshakinywa cha wahudumu pamoja na wengi . . . hapakuwapo na Mpentekoste yeyote, wote walikuwa tofauti, Mwanglikana, na kadhalika. Nao wakauliza kama, nadhani kulikuwa na wengi kwenye hicho

kiamshakinywa sawasawa na wale walioketi papa hapa, kama kamera yao ingeweza kuipiga picha.

Nikasema, "Sijui, Hilo ni la Mungu." Na wengi wao walikuwa wamedai walikuwa wameiona hiyo Nuru. Na kwa hiyo, basi nikasema, "Vema, una . . . "

"Tungeweza kupiga Nuru, au, kupiga picha?"

Nikasema, "Karibuni." Walikuwa na namna fulani ya kamera *kubwa* ambayo iligeukageuka ilipobingirika, loo, kamera nzuri sana, kubwa.

30 Basi ilikuwa yapata saa tano mchana, Nilikuwa nimesimama upande wa mbele wa meza, nikihutubia mamia kadhaa ya wahudumu. Ndipo nilipokuwa nikiwahutubia wahudumu hawa, nilihisi Roho wa Bwana akija, nikasema, "Sasa, Yeye yuaja." Ndipo kamera hiyo ikaanza kupiga picha, moja baada ya nyingine, namna hiyo, papo hapo juu ya mahali nilipokuwa.

31 Nami nikasema, "Mtu huyu aliyesimama hapa na ukosi uliopinduliwa kama wa kasisi," tulikuwa Lausanne, ninaamini wakati huo, badala ya Ujerumani, nikasema, "yeye si Mswisi, wala si Mjerumani," nikasema, "yeye ni Mwitaliano, naye ni kiongozi wa wakomunisti elfu mbili." Kisha nikasema, "Sasa, kusudi aepukane nalo, anajaribu kuendesha kituo kidogo cha watoto yatima huko juu milimani. Sababu ya yeye kutokula kiamshakinywa chake, ni kwa sababu ana ugonjwa wa tumbo."

32 Basi mkalimani alipotafsiri hayo, mtu huyo alizimia tu, akaanguka kwenye sahani yake. Nikasema, "Kula kiamshakinywa chako, kwa kuwa ni BWANA ASEMA HIVI, umeponywa," nikamwambia jina lake lilikuwa ni nani, yale aliyokuwa akifanya. Basi walipochukua hizo picha wapate kuona, walipata—walipata picha Yake akishuka chini, wakati alipokuwa ametiwa upako, na wakati alipoondoka. Loo, jamani, hilo liliondoa ugumu wote kutoka kwa hao wahudumu walioketi pale kuona huo *hapo* ushahidi.

33 Sasa, hebu tuwazie tu kwa muda kidogo, wakati tukiwa wachache tu, nami nina ujumbe mfupi tu, usiku wa leo, kuwazungumzia. Na halafu ningetaka kuuliza jambo hili, ninii tu, hebu tuliwazie tu ka—kama waaminio: Kama Mungu ni Mungu basi hawezi kubadilika, sivyo, ndugu zangu? Yeye hana kikomo, kwa hiyo maamuzi Yake daima hayana budi kuwa makamilifu. Chochote Mungu anachofanyia uamuzi, hakiwezi kubadilika kamwe, kwa sababu alisema Yeye alikuwa ni Mungu, wala hajabadilika. Hebu tuulize swali hili: Nuru hii ingeweza kuwa ni nini?

34 Hiyo, sasa, kumbukeni, si tu kwa sababu yangu mimi, ni Kanisa. Mnaona? Kwangu mimi, ni Kristo.

Mnasema, "Ndugu Branham, ati Kristo akiwa ni Nuru?" Naam.

35 Sasa, tunaona, na hawa wahudumu waliofunzwa vizuri... Nanyi mwajua, usiku wakati ninaposimama mbele ya watu namna hii, ambao kweli wamefunzwa, na ni watu werevu, kwa huduma, na kwa Injili, na kwa Biblia, nami ninasimama hapa nikijua, nikiwa na elimu ya shule ya msingi, kama...Nina kinyongo, kweli. Watu wengi walioketi hapo usiku wa leo, wenye uwezo mwingi mno, ama, wenye uwezo kuliko mimi, kuwa hapa jukwaani, lakini kuwaona wakichukua kiti na kuketi nyuma yangu kuomba, hakika kunalainisha moyo wangu.

36 Sasa, lakini kama tu makasisi, na ndugu, na dada pamoja, tunatambua ya kwamba tunaona ya kwamba katika safari ya nyikani, kulingana na mlango wa 13, naamini ndio, wa Kutoka, vifungu vichache vya mwisho, "Namtuma Malaika Wangu mbele yako, ili akulinde njiani. Mcheni Yeye, kwa kuwa Jina Langu liko ndani Yake, hatawasamehe makosa yenu."

37 Sasa, sote tunajua ya kwamba Malaika huyo alikuwa ile Nguzo ya Moto. Hiyo ni kweli? Ilikuwa ni ile Nuru, Nguzo ya Moto iliyowatangulia wana wa Israeli, iliyowaongoza. Sasa, sote tunajua ya kwamba huyo alikuwa ni yule Malaika wa Agano. Hiyo ni kweli? Ambaye alikuwa ni Kristo. Kwa sababu Kristo alisema vivyo hivyo katika Yohana Mtakatifu 6, walipokuwa wakizungumza, alikuwa akizungumza na Wayahudi pale kwenye ile karamu, Naye...wakasema, "Ulisema umemwona Ibrahimu, nawe bado si Mtu aliyepata miaka hamsini?"

38 Akasema, "Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO. Mimi ndimi ule Mwamba uliokuwa nyikani." Yeye alikuwa ile Nguzo ya Moto, alikuwa Malaika wa Agano, kwa hiyo alikuwa ni Kristo nyikani. Sote tunaamini hilo, sivyo?

39 Sasa, wakati Nguzo hiyo ya Moto, Nuru...Na ni wangapi wanaojua ya kwamba Mungu ni Nuru? Hakika, sawa. Na wakati Mungu alipofanyika mwili, na kukaa katika mwili alioumba, ambao ulikuwa ni Mwanawe wa pekee...Adamu alikuwa mwanawe, mwana aliyeumbwa, bali Yesu alikuwa Mwanawe *aliyezaliwa*. Naye Mungu alikuwa ndani ya Yesu, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Hilo, sote tunaamini hilo, kila Mkristo anaamini hilo, ya kwamba Mungu alikuwa ndani ya Kristo, maana Yeye alisema, "Si Mimi nizitendaye hizo kazi, ni Baba Yangu aishiye ndani Yangu, Yeye huzifanya hizo kazi."

40 Yesu alisema katika Yohana Mtakatifu 5:19, "Sifanyi neno, namwona Baba akilitenda kwanza, na lolote Baba anionyeshalo, hilo ninalifanya. Naye Baba anatenda kazi, nami ninatenda kazi hata sasa."

41 Sasa, tunaona ya kwamba hiyo Nuru basi ilifanyika mwili na kuvaa mwili. Sasa, Yeye alikuwa, Yesu, Mwana wa Mungu, alikuwa na Roho bila kipimo. Hiyo ni kweli? Lakini tunaye kwa kipimo, bali ni Roho yeye yule.

42 Sasa, kama tukiangalia kwenye Siku ya Pentekoste, wakati Roho Mtakatifu aliporudi, hiyo Nguzo ya Moto ndiyo kwanza ijitenge, nazo Ndimi za Moto zikamkalia kila mmoja wao, ndipo wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha kama Roho alivyowajalia kune-. . . Sasa, ndimi, kama ndimi za moto, zilimkalia kila mmoja wao. Ilikuwa ni kitu gani? Mungu, akijigawa Mwenyewe, yule Roho ambapo Yesu alikuwa Naye bila kipimo, na sasa tunaye kwa kipimo, bali ni Roho yeye yule.

43 Kama vile ikiwa ningeenda hapa nje baharini, na kuchota kijiko kimoja cha maji kutoka baharini, vema hiyo isingekuwa ni bahari, lakini kemikali zile zile zilizomo kwenye kijiko hicho zimo katika bahari nzima. Kilicho baharini kiko *hapa* ndani, bali hiki ni ubora ule ule, bali sio kwa wingi. Kwa hiyo sisi, tukiwa na Roho wa Kristo, tunakuwa sehemu ya Kristo. Hiyo ni kweli.

44 Sasa, tunaona ya kwamba wakati Yesu alipokuwa hapa, Yeye alisema, "Nilitoka kwa Mungu, na ninaenda kwa Mungu." Hiyo ni kweli? Sasa, tunaona ya kwamba wakati alipokufa, na kuzikwa, na kufufuliwa tena na Mungu, ameketi kwenye mkono wa kuume wa Mungu, Sauli wa Tarso alikuwa akienda zake Dameski siku moja, naye akabwagwa chini na Nuru, labda, ile Nguzo ya Moto, Nuru, Haikuwa imeonekana kwa mamia na mamia na mamia ya miaka. Naye akabwagwa chini na Nuru hii, kisha Sauti ikalia, "Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?"

Naye akasema, "U nani Wewe, Bwana."

45 Akasema, "Mimi ni Yesu." Alikuwa ametoka kwenye Nguzo ya Moto, akafanyika mwili, akakaa kwetu, akarudi kwenye Nguzo ya Moto, Nuru. Yuyo huyo aliingia gerezani, akamtoa Petro, akamtangulia, akafungua milango, akamtoa nje.

46 Sasa, kama Hiyo ni Nuru ile ile, Roho yeye yule, atafanya Kanisani jambo lile lile alilofanya wakati alipokuwa ndani Yake, kwa kuwa Yeye alisema, "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata ukamilifu wa dahari." Sasa, "Na kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya, nyingi kuliko hizi mtazifanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba Yangu."

47 Kwa maneno mengine, mwili wa nyama, Mwana, asingeweza kuingia ndani ya kila mtu, bali Roho wa Mungu aliyekuwa ndani Yake anaweza kurudi, kwa sababu ni Mungu akijidhili kutoka kwenye Nguzo ya Moto, mtu yeyote aliyeugusa ule mlima hana budi kuuawa, kuchomwa kwa upanga; kisha akafanyika Mtu, akaishi miongoni mwetu, tukamgusa, tukamwamini; alisulubiwa kwa ajili ya dhambi zetu, kisha akafufuka kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu; ndipo kwa Damu Yake yenye haki, tunatakaswa kusudi Mungu aweze kuingia ndani yetu na kufanya ushirika: Mungu akitengeneza njia Yake Mwenyewe

tena ya ushirika pamoja na watoto wa Adamu, kama alivyofanya na Adamu kabla ya kule kuanguka. Nasi tumekombolewa kutokana na laana yote ya kuanguka, na sasa tunayo Arabuni ya wokovu wetu.

48 Kwangu mimi, ndugu zangu, kwangu mimi, si kwa sababu ile Nuru. . . Kamwe hakupigwa picha kwa sababu ilikuwa ni mimi niliyekuwa pale, la, bwana, ni kwa sababu ya Ujumbe wa Pentekoste ninaouwakilisha. Yeye yuko *huko* nje kiasi kwamba, na haidhuru ni karama kiasi gani ingefanya kazi *hapa*, haina budi kufanya kazi *huko* pia. Siwezi kufanya mambo haya bila ninyi, hatuna budi kuwa pamoja kama kitu kimoja, hatuna budi kuwa pamoja.

49 Yesu, wakati alipoenda katika nchi Yake Mwenyewe, kazi nyingi kuu asingeweza kufanya kwa sababu ya kutokuamini kwao, nasi hatuna budi kuamini mambo tuliyotumiwa. Nami najua, ndugu Mkristo, dada, kumekuwa na mambo mengi ambayo yamesemwa ambayo hayakuwa hivyo, bali yachunguzeni tu kwa Maandiko mwone kama ni kweli. Ndipo kama ni Maandiko, naye Mungu ashuhudie jambo hilo, basi hayo ni ya kweli, huyo ni Mungu akinena kwamba ni kweli, kwanza kwa Neno Lake, halafu kwa thibitisho lake, kwamba ni kweli.

50 Kwa hiyo kuhusu ubatizo wa Roho Mtakatifu, kweli ninauamini kwa moyo wangu wote. Ninaamini katika karama zote za Roho, unabii, kunena kwa lugha, kufasiri lugha, na mambo yote makuu yanayoingia katika Mwili wa Kristo. Nami ninaamini kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili huo, na ni washiriki, na raia wenza wa Ufalme wa Mungu, na ndugu na dada wa imani moja yenye thamani. Hivyo ndivyo ninavyosimama, usiku wa leo.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa, kabla hatujasoma somo kwa ajili ya ujumbe mfupi.

51 Bwana mwenye rehema, tunakikaribia kiti Chako cha rehema, Bwana, si kiti Chako cha haki, tusingeweza kukivumilia, Bwana, kwa kuwa hatuombi sheria Yako, hatuombi haki Yako, bali tunaomba rehema Yako. Uturehemu, Bwana, na ukumbuke kwamba sisi ni mavumbi ya nchi, nasi tumetiishwa chini ya makosa ya kila namna, na tunaomba ya kwamba utatusamehe, tunapokiri makosa yetu kwa unyenyekevu.

52 Tunamwombea kila mtu aliye katika Uwepo wa Kiungu, usiku wa leo, ya kwamba Wewe utakuwa hivyo, Mwokozi kwao, na Mponyaji, na Furaha yao, na Amani yao, na Kinga yao, na Ngao yao, na Nanga ya—yao. Tujalie, Bwana.

53 Tunapofungua vifuniko vya Kitabu hiki, mtu yeyote aliye na uwezo kimwili kufungua vifuniko anaweza kufanya hivyo, lakini inahitaji Roho Mtakatifu kulifungua Neno. Tunasoma katika Biblia ya kwamba Yeye aliyekuwa ameketi juu ya Kiti

cha Enzi alikuwa na Kitabu, Nacho kilikuwa kimefungwa ndani na nje, na kutiwa muhuri upande wa nyuma. Wala hapakuwako na mtu Mbinguni, hamna mtu duniani, wala chini ya nchi aliyestahili, ama anayeweza kukitwaa kile Kitabu kutoka katika mkono wa Yeye aliyeketi juu ya kile Kiti cha Enzi. Ndipo akaja Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, Naye akakitwaa kile Kitabu, akaifungua mihuri yake, na kukifungua.

54 Ee Mwana-Kondoo, njoo usiku wa leo, katikati yetu, na kukichukua hiki Kitabu, ukafungue mihuri yake, na kutufungulia Neno, na utulishe kama Mchungaji wetu mkuu, nasi kondoo Wako, tunaotamani *sana* Chakula cha kondoo. Tujalie, Bwana, kwa kuwa tunajua ni Neno Lako. Neno Lako ni Kweli.

55 Tunaomba ya kwamba yule Malaika mkuu wa Mungu, hawa Malaika huku na huko kwenye marefu haya ya kanisa watamshawishi kila asiyeamini, usiku wa leo, kwamba wamekosea. Na kila mtu asiye na Roho Mtakatifu, mvulana au msichana, ama mtoto, jalia wampokee Roho Mtakatifu, usiku wa leo.

56 Waponye wagonjwa na wanaoteseka, jipatie Mwenyewe utukufu. Na ubariki jitihada zetu dhaifu tunapotoa huduma yetu. Katika Jina la Yesu Kristo, na kwa ajili ya utukufu Wake, tunasimama. Amina.

57 Kwa njia ya fungu la maneno, ningetaka kuchukua maneno saba kutoka kwenye ki—kifungu fulani katika Biblia. Na hii, bila shaka, ilikuwa ni Yesu akinena juu ya ndoa na talaka. Lakini sitaki kuliendea hapo, ninataka tu hayo maneno kwa kusudi fulani. Yanapatikana katika mlango wa 19 wa Mathayo, na kifungu cha 8, na maneno saba ya mwisho: *Lakini Haikuwa Hivyo Tangu Mwanzo* [Kiingereza: But It Wasn't So From The Beginning—Mfa.].

58 Kama mkiangalia, kila kitu tulicho nacho siku hizi kilianzia katika Mwanzo. Mwanzo ndio mlango wa chanzo. *Mwanzo* maana yake ni "chanzo." Ndio mlango wa mbegu kwa Biblia. Unaweza kweli kuchukua historia, kama vile *Babeli Mbili* cha Hislop, na waandishi mbalimbali wa kale, na karibu unaweza kulifuatilia Kanisa la kweli, na makundi ya dini potovu, na kila kitu siku hizi, moja kwa moja kutoka Mwanzo, jinsi ilivyotokea, moja kwa moja kutoka kwa Kaini na Habili, uwapandishe juu moja kwa moja, mmoja, mwabuduo na mpinga-Kristo, na huyo mwingine akimwakilisha Kristo, kisha uwalete mpaka Kalvari.

59 Watu wengi huona misalaba mitatu tu pale Kalvari, kulikuwa na minne. Mmoja wao alikuwa ni yule mwizi upande mmoja, mwizi upande huo mwingine, Yesu katikati, halafu Yuda akajinyonga juu ya mkuyu, ambao ni msalaba, "Amelaaniwa mtu aangikwaye juu ya mti." Halafu kulikuwa na Mwana

wa Mungu, aliyetoka kwa Mungu, akimrudia Mungu, huku akichukua pamoja Naye mwenye dhambi aliyetubu; yule mwana wa upotevu akitoka kuzimu akirudi kuzimu, akimchukua yule mwenye dhambi asiyetubu.

60 Na yapata tu wakati Kristo alipomwaga Roho Wake Mtakatifu, alipojitokeza jukwaani, mpinga-Kristo akajitokeza jukwaani; yapata tu wakati, katika siku hizi za mwisho, Roho Mtakatifu anapoanza kujifunua Mwenyewe, mpinga-Kristo anajifunua mwenyewe; na yapata wakati wa kuja kwa Kristo, mpinga-roho anakuja pia, roho ya mpinga-Kristo. Kwa hiyo tunaona wanafanya kazi pamoja, Yesu alisema, "Watafanana sana, hata ingewapoteza walio wateule, kama yamkini."

61 Sikubaliani na Ndugu yetu mashuhuri, maarufu Billy Graham katika ujumbe wake hivi majuzi, alisema ya kwamba mpinga-Kristo tayari amewadanganya walio wateule, bali siamini hilo, kwa sababu haiwezekani, walichaguliwa na majina yao yakaandikwa katika Kitabu cha Uzima kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, wakati Mwana-Kondoo alipochinjwa.

62 Sasa, kwamba ni nani, sijui mimi. Mnaona? Lakini Mwana-Kondoo alichinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, naye mpinga-Kristo atawadanganya wote walio juu ya nchi ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Kwa hiyo mnaona, tunavuta na kuwavua samaki tukijaribu kuona mahali hao watu walipo, yule ambaye jina lake liliwekwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. "Wote aliotangulia kuwajua aliwaita, wale aliowajua. . .aliowaita, aliwahesabia haki, wale aliowahesabia haki, tayari amewatukuza."

63 Kwa hiyo tunaogopa nini? Jambo ni kwamba, unasema, "Vema, tutaishi vivi hivi tu," hiyo inaonyesha ya kwamba jina lako haliko kwenye kile Kitabu. Hiyo ni kweli kabisa. Hiyo inathibitisha kwamba hukuandikwa, unapojaribu kuishi maisha ya namna yoyote, na, unayotaka kuishi, hiyo inaonyesha hujampata. Kama wewe ni Mkristo halisi, utaishi Maisha halisi, kwa sababu Uzima wa Kristo uko ndani yako, nawe huwezi kufanya jambo lingine ila kuishi Maisha ya Kristo.

64 Sasa, tunaona hapo mwanzo. . .Nilikuwa nikishuka kuja barabarani alasiri ya leo, nami nikaona ya kwamba jiji hili ndilo linalosifiwa sana kwa *Mahindi Chotara Ya Funk*. Mahindi chotara, jinsi yalivyokuwa. . .Nimeyaona kote nchini, naamini ndiyo, *Mahindi Chotara ya Funk*. Nami nilikuwa nikishuka kwenye 150 alasiri ya leo, nami, ama, leo, yapata adhuhuri, ndipo nikaona, kasema, "Bloomington, Illinois, nyumbani kwa *Mahindi Chotara ya Funk*." Nami nikawazia, "Vema, sasa hilo ni ja—jambo kubwa, ni mahindi mazuri, bali hayafai kitu." Si mazuri hata kidogo. Chochote chotara sio sawa, ni kitu

kilichopotoshwa, na si—si asili yake. Na chochote ambacho si cha asili sio sawa. Mungu alifanya kila kitu sawa hapo mwanzo.

65 Na sasa, ningetaka tu kupitisha hili, kwa kuwa niko shuleni, nami ningetaka mtu fulani aelezee hili: Mnajua, tunaambiwa kwamba tulikuja, na kwa mageuzi yanayoendelea tumekua kutoka kwa kiluwiluwi tukawa tumbili, kisha tukawa mwanadamu. Huo ni wazimu jinsi gani, wakati Mwanzo mlango wa kwanza, na kifungu cha 11, Mungu alisema, "Kila mbegu na izae kwa jinsi yake." Ukiizalisha hiyo mbegu, inaiua papo hapo, kamwe haiwezi kupata kitu kingine chochote ila hicho, hiyo ni kweli kabisa. Unaweza kuyachanganyia mbegu mahindi, hiyo ni kweli, na kufanya suke zuri, kubwa la mahindi, lakini huwezi kupanda mahindi hayo na kupata mahindi mengine chotara. Imekwisha mara tu inapozaa mazao yake ya kwanza, inarudi moja kwa moja tena.

66 Kuzalisha mifugo, unaweza kumchukua nyumbu... Nyumbu ni nini? Nyumbu ni kwamba mama yake alikuwa farasi jike, baba yake alikuwa punda. Kwa hiyo mnaona, ninii... Lakini nyumbu hawezi kuzaa tena na kupata nyumbu, amekwisha, yeye ni tasa, hivyo tu, hiyo inaishia hapo.

67 Kwa hiyo hilo linathibitisha kwamba sayansi, ikitenda kazi katika uwanja wao wenyewe, imekanusha hoja yao wenyewe. Hiyo ni kweli, ni kweli, maana huwezi kuchanganya kitu kama hicho na—na kupata mazao mengine kutoka kwake, ninyi wakulima mnajua hivyo. Mahindi yenu chotara hayawezi kupandwa tena, hamna mazao, hayafai kitu. Hatimaye, inajimaliza kabisa. Hakuna chochote chotara kinachoweza—kinachoweza kudumu.

68 Lakini imekuwa ni wazo la mwanadamu tangu mwanzo kabisa kujaribu kushinda kwa akili, au kufanya jambo kubwa kuliko Muumba wake. Anataka kuwa... anataka kumwonyesha Muumba wake kwamba yeye ni mwerevu kuliko Yeye alivyo. Anafanya nini? Ninii tu, Mungu humwachilia, kisha hatimaye anajiua.

69 Kulikuwa na mti katika bustani ya Edeni ulioitwa Mti wa Uzima, kulikuwa na mmoja ulioitwa Mti wa Maarifa. Wakati mwanadamu alipouacha huo Mti wa Uzima, ambapo alikuwa akila apate kuishi milele, mmego wa kwanza aliouma wa huo Mti wa Maarifa alijitenga na Mungu, na kuleta mauti kwa nafsi yake. Hiyo ni kweli. Na tangu wakati huo, kila wakati anapouma Mti huo wa Maarifa, anajiangamiza mwenyewe.

70 Aliuma baruti, anamwua ndugu yake, mwenziwe. Aliuma motokaa, sayansi. Anafanya nini? Anaua watu wengi kuliko vita vyote vikiwekwa pamoja. Amejipatia bomu la haidrojeni sasa, sijui atafanya nini nalo.

71 Mnaona, mwanadamu hujiangamiza mwenyewe kwa maarifa, naye kamwe, kwa elimu ama maarifa, kamwe hatapata

njia ya kumrudia Mungu. Na mti huo, anakufia karibu na mti huo. Tumejaribu kuingiza watu kwake kwa elimu, tumejaribu kuingiza watu kwake kwa kuwaundia madhehebu, huwezi kufanya hivyo, hatuna budi kumtanguliza Mungu kwanza, mpango wa asili, kwa Damu tunamrudia Mungu. Hiyo ndiyo njia ya Mungu na ninii Yake... Yeye aliuweka msingi huo katika bustani ya Edeni, nao haujawahi kubadilika, na kamwe hautabadilika. Ni kwa damu iliyomwagika tu ambapo Mungu atatambua upatanisho wa mwenye dhambi, ni kwa Damu iliyomwagika ya Yesu Kristo sasa.

72 Sasa, tunaona, lakini sikuzote yeye hujaribu kumshinda akili, kufanya jambo bora zaidi. Na ni kweli, yeye anafanya spishi nzuri zaidi, lakini hiyo haiifanyi bora zaidi. Naye amewaza akawazua sasa, mpaka hata ana dini chotara, kwa hiyo nashangaa tu atafanya nini nayo, ambapo amefikia mahali hapo. Lakini daima yeye hujaribu kumshinda akili Muumba wake. Anafikiri kwamba anajua vizuri zaidi, na—naye ni . . .

73 Wala Mungu kamwe haharibu chochote, mwanadamu hujiangamiza mwenyewe kwa maarifa yake. Mungu haharibu chochote, ni mwanadamu, kwa maarifa yake, hujiangamiza mwenyewe. Kwa hiyo, basi kama ungechukua muda, urudi katika Maandiko, na kufuatilia ukoo wa Kaini halafu ukoo wa Sethi, utaona ya kwamba watu wa—wa ukoo wa Kaini walikuwa werevu, wanasayansi, wafanyakazi wa mbao, wafua chuma, wanasayansi, nao wote wakaangamia katika yale maangamizi yaliyotangulia ile gharika kuu. Lakini ukoo wa—wa Sethi walikuwa wanyenyekevu, wakulima, wafuga kondoo.

74 Kwa hiyo mnaona, daima ni watu hawa, ambapo siku hizi tunatilia mkazo sana wenye akili na werevu, wengi wetu watu tunapomchagua mchungaji wetu kwa kanisa letu, tunataka mtu ambaye kweli ni mwerevu sana, mwenye akili, aliye na Ph.D., L maradufu D., Q.S.T., vitu vya kila namna nyuma ya jina lao, na labda hawajui zaidi kumhusu Mungu kuliko Mhotentoti anavyojua kuhusu hekaya za Kimisri. Sasa, hiyo ni kweli. Sasa, hilo ni tamshi fidhuli, samahani kwa hilo tamshi fidhuli, bali hiyo ni kweli. Huenda akajua theolojia ya Biblia na kanuni za imani za kila namna, bali hajui chochote kumhusu Mungu.

75 Afadhali mtu akae na mtoto wangu, akimwongoza kwa Mungu, mtu ambaye hakujua tofauti kati ya maharagwe yaliyopasuliwa na kahawa, na—na anamjua Mungu katika nguvu za kufufuka kwa Yesu Kristo, kuliko kuwa na theolojia yote ambayo ungeweza kuzungumzia, na kumpelekea kiti kikubwa cha kifahari mahali fulani, umpigishe magoti, na kunena mambo machache, Afadhali nimweke huko nje kwenye shamba la mahindi, ama kwenye kichaka kidogo karibu na kisiki mahali fulani, nikimwombea amfikie Mungu. Hiyo ni kweli. Rudini kwenye ya asili. Kamwe hatumjui Mungu . . .

76 Miaka michache iliyopita, walidhani wangeweza kuwaelimisha watu. Nasi tuna nini sasa? Kundi la makafiri wenye elimu. Ni kweli kabisa. Nao ni wagumu sana kushughulika nao kuliko makafiri wasio na elimu.

77 Sasa, nimekuwa huko Afrika, nami nimefanya umishenari huko Thailand, na kote ulimwenguni, karibu kila taifa chini ya mbingu, wala maishani mwangu sijawahi kuona watu wagumu kushughulika nao kuliko huku Marekani. Kama kuna mahali popote ambapo kweli wanahitaji mmishenari ni Marekani, maana kafiri ni asiyeamini, na mwenye elimu asiyeamini ni mgumu zaidi kushughulika naye kuliko mtu asiye na elimu. Sasa, hilo, sisemi hilo ili kuwa fidhuli, lakini huo ndio ukweli, nami ninawajibika na nitawajibika kwenye Siku ya Hukumu kwa ajili ya maneno yangu. Hiyo ni kweli, mwanasayansi mwerevu, mwenye akili, asiyeamini, hata hivyo ni wa kidini kwelikweli, ndivyo alivyokuwa Kaini.

78 Ikiwa Mungu anataka tu mtu kwenda kanisani, ajenge madhabahu, na kuabudu, Kaini alihesabiwa haki tu sawasawa na Habili, wavulana wote wawili walijenga madhabahu, wavulana wote wawili waliabudu, wote wawili walitoa dhabihu, wote wawili walimwamini Mungu. Lakini ilikuwaje? Ya Kaini ilikataliwa kwa sababu hakuja kwa njia iliyowekwa na Mungu. "Na iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti."

79 Haijalishi unajaribu kiasi gani kwenda kanisani, wewe ni wa makanisa mangapi, hilo halina uhusiano wowote nalo, halimaanishi chochote kwa Mungu, hata haimaanishi hata umeanza kwenye msingi wa kwanza wa wokovu. Wokovu hauji kwa madhehebu wala kwa elimu, huja kwa tukio la kuzaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, huku Roho wa Kristo akiishi katika mwili wako. Sasa, hiyo ni kweli.

80 Sasa, tunaona ya kwamba huko nyuma hapo mwanzo, wakati watu walipoanza kujaribu kupotosha kile Mungu alichokuwa ameumba, mwanadamu hujaribu kupotosha ili kukifanya maridadi zaidi, kukifanya kivutie zaidi. Na laiti ningalikuwa na wakati wa kuwaelezea tu, kile kinachotendeka juu ya upotovu.

81 Mnajua ni kitu gani kinachosababisha kansa? Chakula kilichopotoshwa. Hiyo ni kweli kabisa. Kile. . . Wao wanasema, wanasayansi wanadai ya kwamba katika miaka ishirini zaidi kama wakiendelea kuwaruhusu wanawake kula kuku, na kadhalika, hao ni hawa kuku chotara, na kadhalika, kwamba hawataweza kupata watoto tena; hii jamii itakwisha kwa sababu mwanamke hawezi kumzaa mtoto.

82 Ni kitu gani kimetukia kwa upotovu? Tunapaswa kula punje asili ya kitu chochote. Lakini jambo ni kwamba, ulimwengu sasa, taifa lilivyo, liko tu katika hali ya upotovu mkubwa mno. Wa—

wamechukua kuku na kuwachanganyia mbegu, na kadhalika, na kufanya kuku chotara, mpaka maskini huyo kuku anaweza tu kuishi mwaka mmoja tu. Nyama yake ni nyororo sana, naye alimfanya hivi kwamba hata hana mabawa yoyote, au, machache sana. Mbona, yuko katika hali mbaya sana! Na wao—wao—wao wanakulisha nyama hiyo, ng'ombe chotara, na kadhalika. Lakini hiyo si . . . Hao kuku hawawezi kujizalisha tena, wala hao ng'ombe. Wao ni chotara, hawawezi, wamekwisha. Kweli kabisa.

83 Na wakati kanisa linapokuwa chotara, limekwisha, limefagiliwa mbali. Simaanishi kuwa fidhuli, lakini sina budi kuwa mwaminifu, huenda nisikutane na yeyote wenu, uh, baadhi yenu hapa tangu usiku wa leo na kuendelea, huenda tusione kuja kwa asubuhi, lakini basi tunataka kuwa waaminifu, na kila dakika ya maisha yetu inabidi tuwe waaminifu.

84 Mchukue nyumbu, nyumbu ndicho kitu kijinga kuliko vyote nijuacho. Haidhuru utawahi kufanya nini, huwezi kumfundisha chochote. Kwa nini? Yeye ni chotara. Hivyo tu. Yeye . . . Kamwe hutamfanya ajifunze chochote, wala kumfundisha chochote, anaketi tu hapo. Unaweza kumwita, yeye hana upendo, atasimama pale huku ameyainua masikio yake na, "Hoo, hoo." Hajui, yeye ni punda tu, yeye ni nyumbu.

85 Inanikumbusha baadhi ya watu, baadhi ya dini hii ya nyumbu waliyo nayo siku hizi, ya kisasa, ya ajabu, dini chotara, kama kundi la punda lilivyoketi, na kusema, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye ni Mponyaji, Yeye hutoa ubatizo wa Roho Mtakatifu," watapiga makelele, "*Hoo*, *hoo*, siku za miujiza zimepita, *hoo*, *hoo*." Mnaona, hawajui walikotoka. Nyumbu hajui mama yake ni nani, baba yake ni nani, naye amekwisha kwa vyovyote vile. Hajui, hana chochote, yeye ni—yeye ni, ni kitu haramu tu.

86 Na hivyo ndivyo baadhi ya dini zetu zinavyokuwa. Hiyo ni kweli. Hawaijui Biblia, hawamjui Mungu, jambo pekee wanalojua ni ya kwamba kuna mahali pa namna fulani tu unapohudhuria kanisa, mtu fulani aliwaingiza kama wafuasi, wakaleta barua yao kutoka kwa kanisa *lingine*, ndipo wakawaingiza kwenye kanisa *hili*. Wataketi mkutanoni kwa dakika chache mpaka utakaposema jambo wasilolipenda, na hata hawana malezi mazuri, ya adabu, wataamka na kutoka nje, huo hata si Umarekani.

87 Mama yangu alinilea kwa akili nzuri kuliko hizo. Kama ningehudhuria mkutano, ningekuwa muungwana kutosha kuketi kimya na kusikiliza, la sivyo kwa kuanzia hata nisingeuhudhuria. Hiyo ni kweli. Hilo hata halionyeshi malezi mazuri. Si ajabu tuna uhalifu wa vijana, tuna uhalifu mwingi wa wazazi uliousababisha hilo. Hiyo ni kweli.

88 Sasa, ni aibu jinsi gani juu ya kanisa, na juu ya Kristo, na juu ya huduma! Naam, nyumbu, yeye ni maskini chotara mjinga,

hajui chochote, ila tu anajua . . . Naye atangojea maishani mwake mwote apate kukupiga teke wakati akifa, hiyo ni kweli, mtu yeyote anayejua lolote kuhusu nyumbu.

89 Lakini, loo, ninampenda farasi mzuri wa ukoo safi, hakuna chochote chenye sura nzuri zaidi. Yeye ni ukoo safi, anajua baba yake alikuwa ni nani, mama yake alikuwa ni nani, babu yake alikuwa nani, kwamba babu wa babu yake alikuwa ni nani, yeye ni ukoo safi.

90 Nami ninapenda kuona kanisa zuri kweli, la ukoo safi, na Mkristo anayejua Baba yao ni Nani, anayejua ya kwamba Mungu ni Baba yao, anayejua ya kwamba wamezaliwa na Roho Mtakatifu, wanaweza kuufuatilia huko nyuma katika kila kizazi, huko nyuma kabisa hata mwanzoni. Sio, "Tulianza wakati Luther alipoanza. Tulianza wakati Wesley alipoanza. Tulianza wakati mtu mwingine alipoanza." "Tulianza wakati Kristo alipomwaga Roho Wake kwenye Siku ya Pentekoste," ukoo safi. Amina. Ndugu, ukinena Neno la Mungu, anaweza kuitikia, "Amina," kwake. Hebu na ampokee Roho Mtakatifu, atatenda hasa kama walivyofanya hapo mwanzo, kwa sababu yeye ni ukoo safi.

91 *Whiu*! Kwa namna fulani ninajisikia kubarikiwa sasa hivi. Naam, amina. Huchukizwa sana na upuuzi huu mgumu. Ninapenda dini halisi, nguvu halisi, halisi za Mungu, mnaona. Kwa nini itubidi kuwa maskini hawa punda chotara waliochanganyikana na mambo ya kila namna, wala hatujui tunakotoka, sisi ni wa nini? "Kama Wamethodisti hawatutendei mema, tutajiunga na Wabaptisti. Wabaptisti wasipotutendea mema, tutaenda kwa Wapresbiteri, ama mahali pengine."

92 Hebu turudi Kalvari na kupata ukoo halisi wa Roho Mtakatifu ndani yetu, ndipo unajua mahali unaposimama, unajua Baba yako ni Nani, na kila wakati basi, Biblia inaposema lolote, unaliitikia kwa, "Amina." Biblia ilisema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, na hata milele."

Maskini punda anasema, "Sijui kuhusu hilo."

93 Lakini ukoo safi halisi, wa kweli unasema, "Amina!" Naam, bwana, yeye ni ukoo safi. Kuzaliwa kwake kulitokea kote kote huko Pentekoste, kote kote chini, kwa hiyo anajua mahali anaposimama. Yeye ni mtu halisi, wa kweli wa Mungu, aliyezaliwa na Roho Mtakatifu, akaoshwa katika Damu ya Mwana-Kondoo.

94 Maskini Kanisa hilo limepitia miaka elfu moja mia tano katika nyakati za giza, mpaka likawa katika uchache kabisa. Nilikuwa nikizungumza na kasisi fulani hivi majuzi aliyekuwa akihoji, akasema, "Tulianzia Pentekoste."

95 Nikasema, "Hiyo ni kweli kabisa, lakini kwa nini mkaondoka, ndiyo ninayotaka kujua. Ilikuwaje mkapoteza?" Nikasema, "Yale waliyofundisha huko nyuma, kama huyo

alikuwa ndiye papa wa kwanza, Petro alikuwa, basi kwa nini sivyo mlivyo siku hizi?"

Kasema, "Vema, tuna ondoleo la dhambi. Tunaamini ya kwamba Yesu alisema, 'Wowote mtakaowaondolea dhambi, wameondolewa.'"

96 Nikasema, "Hiyo ni kweli." Nikasema, "Basi ziondoeni jinsi papa wa kwanza alivyofanya kwenye Siku ya Pentekoste. Ndipo mimi," nikasema, "Mimi ni wa mtindo wa kale, mimi ni Mkatoliki wa mtindo wa kale." Nikasema, "Ilikuwa ni nini? Katika wakati wa pili wa kanisa walipata kile wanachokiita 'matendo,' Yesu alisema, 'ya Wanikolai.' *Nikao*, 'kuwashinda' walei. Na katika wakati wa tatu basi, wa Smirna, wakati wa ndoa. Ndipo ukaja wa Thiatira, nao wakaunda dhehebu kubwa mno, na kuliweka sawa, na kuondoa kila kitu, ndipo kundi hilo dogo la waaminio wa kweli wa Kipentekoste likakanyagiwa chini."

Akasema, "Mbona, inathibitisha ya kwamba kanisa Katoliki ni kanisa kuu, angalia dhoruba kubwa zilizolikabili."

97 Nikasema, "Likiwa na—likiwa na serikali na kila kitu nyuma yake, na watu wote mashuhuri? Hilo si fumbo. Wapentekoste *walililihuishaje* huku wakipingwa na kila kitu ila Mungu?" Amina. Lakini tungali tunasimama na ubatizo wa Roho Mtakatifu.

98 Kwa nini unataka kuchukua kibadala wakati mbingu zimejaa nguvu halisi za Kipentekoste? Kwa nini nichukue kupeana mkono, ama maungamo ya macho makavu, wakati Roho Mtakatifu anapokijaza chumba, na yuko tayari kuujaza moyo wako na Pentekoste halisi, ya kweli? Kwa nini tuchukue kibadala chake? Acha niwe na Kristo. Amina, kweli.

99 Na kama Uhai wa Kristo uko ndani yako, utafanya jambo lile lile. Hilo lilikuwa ndilo kanisa kielelezo cha Mungu, lilikuwa ni Pentekoste. Kama tunadai kuanza kutoka hapo, basi ni jambo gani limetukia? Ni kitu gani kilichotukia njiani? Tutalifikia baadaye, kama mtanivumilia tu kidogo.

100 Sasa, angalieni, sasa, tunaona ya kwamba katika kanisa hili kuu, wakati huu mkuu wa upotovu, walawiti, nilichukua jarida, ama, halikuwa jarida, lilikuwa ni gazeti la kila siku huko California majuma machache yaliyopita, nilipokuwa huko Los Angeles, nao wakasema kwamba walawiti walikuwa wameongezeka kwa asilimia arobaini. Wazieni jambo hilo, asilimia arobaini kuliko vile ilivyokuwa miaka michache iliyopita. Ni kitu gani? Upotovu. Wanaume, wanawake, kila kitu kinapotoka. Sio kurudi kwa ya asili tena. Maisha ya kila siku, ya kawaida yamebadilika ndani ya mwanadamu, nia yake imebadilika, roho yake inabadilika, amebadilisha kila kitu kutoka cha asili. Loo, si ni jambo la kusikitisha? Ni ninii sana . . .

101 Vema, hivyo ndivyo Biblia ilivyosema hasa, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Mungu hawezi kumwaga Roho Wake juu ya watu wenye haki na awe mwenye haki, hawana budi kuingia katika hali hii kwa ajili ya hukumu za Mungu. Nasi karibu tuko hapo sasa, enyi marafiki. Kama mkishikilia tu juma lote lililosalia, labda Bwana atalifunua, nasi tutaona kile. . . jinsi tulivyo karibu, moja ya siku hizi usiku, na Kuja kwa Bwana. Kamwe msiwazie juu ya umati mkubwa, ni uchache, ni Kanisa dogo ambalo Mungu analifuatilia, kumbukeni hilo. Vema.

102 Hawa alikuwa wa kwanza kuipotosha jamii ya binadamu, alikuwa ndiye, Hawa, ambaye anawakilisha kanisa. Mwanamke katika Biblia daima huwakilisha Kanisa. Kristo anakuja kwa ajili ya bikira aliyeposwa. Yule kahaba wa kale wa Biblia aliitwa, “kanisa lililoketi juu ya vilima saba,” kanisa la Kirumi, hata hivyo, kanisa, naye alikuwa na binti, ambao walikuwa hao wengine waliomfuata kisha wakatoka kwake, waliozaliwa naye, katika vizuizi vyao vile vile vya kimadhehebu na kitu kile kile, mfumo wa namna ile ile.

103 Ndani ya makanisa hayo mna watu wazuri, bali ni mfumo ndio unaowafunga, si kanisa lenyewe, ni, hao watu kanisani, ni huo mfumo ulio nyuma yake unaowafunga, unawaingiza mahali fulani, unavunja ushirika, hautawaacha waendelee pamoja na Mungu. Ni jambo la kusikitisha, lakini hivyo ndivyo ufanyavo. Hicho ndicho Mungu anachochukia, sio watu mle ndani, bali huo mfumo unaowafunga ndio anaochukia, ni dhehebu hilo linalowaambia kama wakihudhuria kanisa lingine watatengwa, nao hao watu hawajui la kufanya. Watalijutia siku moja.

104 Lakini Hawa, alipotoshwaje akaanzisha dini potovu? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kwa kitambo kidogo. Ni kile alichofanya. Shetani alimpa Neno la Mungu *kidogo*.

105 Hivyo ndivyo hasa Shetani alivyojaribu kufanya wakati wote, hivyo ndivyo anavyofanya usiku wa leo, hivyo ndivyo anavyofanya katika shule za Biblia, hivyo ndivyo anavyofanya katika seminari hizi za kitheolojia, yeye hutoa Neno kidogo kisha anaongeza neno la kujibunia ndani yake, ni kweli kabisa, ambalo linaifanya dini chotara.

106 Loo, tuna makanisa mazuri zaidi, hakika, umati uliovalia vizuri zaidi, wenye elimu ya juu sana, wakiwa na wahubiri wenye digrii za chuoni za kila namna, na mambo kama hayo. Lakini tufanye nini? Hatuwezi kurudi kwenye lile la Asili tena, kwa sababu huwezi kujirudisha mwenyewe, si zaidi ya vile nyumbu anavyoweza kurudi. Hamna budi kuzaliwa mara ya pili kama watu binafsi, kwa Roho wa Mungu hapo Pentekoste, hiyo ni kweli, ile baraka iliyoshuka.

107 Pentekoste si dhehebu, Pentekoste ni tukio linalowajia Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, Wakatoliki, "Yeyote atakaye, na aje." Pentekoste si dhehebu, huwezi kuundia dhehebu baraka za Mungu. Ni bure kwa mtu yeyote atakayekuja na kulipokea, nao wanatoka katika matabaka mbalimbali ya maisha, na makanisa yote mbalimbali.

108 Lakini Hawa alijaribu kuchukua baadhi ya mambo ambayo Shetani alimwambia, baadhi ya mambo ambayo Mungu alimwambia, na kutenda kulingana na tendo lilo hilo, na hapo ndipo alipopotea, hapo ndipo alipofanyika chotara. Ndipo uzao wa Shetani ukaja, ungali unaendelea, uzao wa Shetani. Kitu hicho ni ninii sana. . . Chotara ni kitu kiovu sana machoni pa Mungu!

109 Katika Agano la Kale mtoto aliyekuwa chotara, aliyezaliwa nje ya ndoa takatifu, asingeweza hata kuja katika kusanyiko la Bwana kwa vizazi kumi, ilichukua vizazi kumi kulisafisha. Hiyo ni miaka mia nne ya kumalizia uzazi wa mtoto haramu, asingeweza hata kuingia katika kusanyiko la Bwana. Kuchanganya mbegu, mwanamke aliyeweka nadhiri kwa mumewe, na kuishi na mwanamume mwingine, na kuzaa mtoto naye, jambo la kuchukiza sana!

110 Siku hizi, tunazozana sana na kugombania ubaguzi huu wa watu weupe na weusi, na kila kitu. Kwa nini wasiachane nao? Hebu iwe jinsi Mungu alivyoifanya. Niambie ni mwanamke gani mweusi, halisi, mzuri, mwerevu, mwenye akili angetaka kumzaa mtoto na mzungu apate kumfanya chotara? Si busara. Vitu vingi walivyo navyo watu weusi vimeshinda vya mzungu kwa mbali.

111 Ninawazia juu ya yule mhudumu mweusi, aliyesimama kule chini siku hiyo huko Shreveport, akasema, "Kamwe sikuona aibu kuwa mtu mweusi. Mungu aliniumba mtu mweusi, nami ninamthamini Muumba wangu aliyeniumba namna hii, ndivyo alivyonikusudia. Lakini," kasema, "leo, kuona watu wangu wakitenda jinsi wanavyotenda, basi ninaona aibu mimi ni mtu mweusi." Mungu aubariki moyo wake mwaminifu. Bila shaka.

112 Mwanamke mweupe angetaka kumzalia mtoto mwanamume mweusi kwa nini, kumfanya chotara? Si busara. Kama Mungu alitaka mtu wa kahawia, mweusi, mweupe, rangi yoyote aliyomtaka, huo ni uumbaji wa Mungu, hivyo ndivyo alivyotaka. Anataka maua meupe, maua ya samawati; Mungu ni Mungu wa namna mbalimbali. Anapenda milima mikubwa, milima midogo, majangwa, nyanda, mweupe, mweusi, mfupi, mnene, na asiyejali. Mungu ni Mungu wa namna mbalimbali.

113 Kama ningalikuwa mtu mweusi, ama mtu wa hudhurungi, ama mtu wa manjano, ama mtu mwekundu, ningefurahia tu hilo. Naam, bwana. Hakika ningefurahia. Hivyo ndivyo Muumba wangu alivyonitaka na hivyo ndivyo nilivyo. Sawa. Kwa nini mwanadamu anataka kuharibu chochote? Mwanadamu

anapokiingilia, anakiharibu. Achana nacho, jinsi Mungu alivyokiumba. Mtu na awe jinsi alivyo, kwa neema ya Mungu na awe.

114 Lakini hana budi kusababisha vurugu kubwa sasa, akiita ninii yetu. . . akisababisha ghasia, na mizozo mikubwa, na kadhalika kote katika mataifa, na kote ulimwenguni, kwa sababu tu alitaka kutokeza kichwa chake kuhusu jambo fulani, huo ndio ujinga wa huyo mtu, hiyo ni kweli, chotara tena. Badala ya kuliacha jinsi Mungu anavyolitaka, yeye anataka kufanya njia yake mwenyewe. Hana budi kufanya jambo fulani kulihusu, mwajua, hana budi kujifanyia mwenyewe jina. Mungu amrehemu, ni jambo la kusikitisha.

115 Vema. Sasa, lile Neno ambalo Mungu alimwambia Hawa, ndipo Shetani akaja na kukubali kwamba sehemu hiyo ya Neno ilikuwa ni kweli, lakini akasema, "*Hakika* sehemu hii si sawa."

116 Sasa, hilo si ni kama vile baadhi ya seminari za kitheolojia zinavyofundisha siku hizi? "Loo, kuna Mungu. Tunamwamini Yesu. Hakika, Yeye ni Mwana wa Mungu, ninaamini hilo. Loo, ninaamini katika kuonekana Kwake dhahiri. Lakini sasa, atakapokuja kuwa ni Mponyaji, ama upuuzi huo wote wa Roho Mtakatifu, uh, ah, ah, huh-uh." Mnaona, huo ni uchotara ule ule. Biblia ilinena juu yao, ikasema watakuwa katika siku za mwisho, wakaidi, wenye kujivuna.

117 Hapa si muda mrefu uliopita nilialikwa kuzungumza kwenye shule fulani, walipogundua kwamba nilikuwa na elimu ya darasa la saba, kasema, "Loo, tusingeweza kumweka huyo mbele ya wanafunzi wetu." Wasingeweza kuliweka mbele ya hao wanafunzi.

118 Jinsi ilivyokuwa tofauti na Paulo! Paulo alisema, "Sikuja kwenu kwa hekima ya wanadamu, maneno ya kushawishi, ili imani yenu ijengwe juu ya hekima ya wanadamu, bali nilikuja kwenu kwa nguvu, na dhihirisho la Roho Mtakatifu, ili imani yenu ijengwe katika Mungu." Leo hii, leo hii wanataka kufanya shule ya elimu kutoka kwake, kusoma, na kuandika, na hisabati.

119 Nilipofika Afrika miongoni mwa ndugu zangu weusi, walijua nini? Kusoma, kuandika, na hisabati, hawakuwa na shughuli na hilo. Hiyo ndiyo sababu walipomwona Mungu halisi, wa kweli, anayetenda kazi akija miongoni mwa watu, thelathini elfu walimkubali Kristo kwenye wito mmoja wa madhabahuni, Durban, Afrika Kusini. Kile kitabu kinaelezea hayo. Mnaona? Hiyo ni kweli.

120 Bombay, India, labda kulikuwa na watu laki tano waliohudhuria mkutano huo, ni vigumu kusema ni wangapi waliokuja kwa wakati mmoja. Si kusoma, kuandika, na hisabati, huwaleti watu kwa Mungu kwa njia hiyo, ni Injili. Injili kamwe haiji kwa Neno tu, bali kwa nguvu, na madhihirisho ya Roho Mtakatifu. Yesu alisema, "Enendeni ulimwenguni kote,

mkaihubiri Injili. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Inahitaji zaidi ya kufundisha Neno tu, inahitaji dhihirisho la Neno hilo kuzifanya ishara hizi zifuate, hiyo ni kweli, Mungu akijidhihirisha Mwenyewe.

121 Mtu fulani alisema, "Vema, njoo, kwa nini usifanye *hivi*, kwa nini usifanye *vile*?" Vema, ndugu, afadhali niwe huko nje nikifanya kosa, nikijaribu kufanya jambo fulani vizuri, kuliko vile ningekuwa nikijaribu kuwanyang'anya watu tumaini la mwisho walilo nalo. Kama nikifanya kosa. . .Niliwaombea mamia ya watu ambao hawakupata afya, lakini afadhali niwe nikiwaonyesha watu hao Mungu, na Biblia, na Kristo aponyaye, kuliko kujaribu kuwanyang'anya nafasi ya mwisho waliyo nayo ya kupata afya.

122 Kusema unawapenda wanadamu na huku unawaficha vitu hivyo, itakuwa kama kumpa, kujaribu kumpa maziwa mtoto anayekufa, kisha kumnyang'anya. Si sawa, kuna kasoro fulani. Sababu ya kufanya hivyo ni kwa uchotara, kwa sababu wanakubali ya kwamba kanisa lao litawafukuza kwa ajili ya jambo hilo, kweli, chotara. Naam, Neno, wala usilichanganye Neno na chochote.

123 Unajua, Shetani alijaribu hilo juu ya Yesu wakati mmoja. Loo, naam. Wakati mmoja alikuja Mtu kutoka Mbinguni kubadilisha hali hii ya uchotara. Kwa hiyo kama vile alivyomjaribu Hawa, yeye pia alimjaribu Yesu, akampandisha juu ya mlima, akasema, "Sasa, *kama* wewe ni Mwana wa Mungu, ninataka ufanye mwujiza ili niweze kukuona ukiufanya." Maskini ibilisi yuyo huyo anaishi leo, ndani tu ya watu wengine; Roho yuyo huyo wa Kristo anaishi leo, ila tu katika watu wengine, mnaona, kweli. Mtu huyo huondoka, bali Roho kamwe haondoki.

124 Kwa hiyo basi akampandisha juu ya mlima, akasema, "Sasa, *kama* wewe ni Mwana wa Mungu," akamjaribu kwa Neno, kasema, "imeandikwa katika Biblia, 'Atakuagizia Malaika Zake, usije ukajikwaa mguu Wako katika jiwe, watakuchukua,'" mnaona, sehemu ya Neno.

Lakini Yeye hakujikwaa mguu Wake katika jiwe, kwa hiyo akasema, "Na pia imeandikwa!" Amina.

125 Loo, alijua alikuwa na Mtu fulani pale mbali na Hawa wakati huo, asingeweza kumchanganyishia Huyu mbegu. La, bwana. Kwa nini? Yeye alikuja kuizalishia tena jamii ya Adamu imani iliyo hai katika Neno lililo hai la Mungu aliye hai. Naye alithibitisha papo hapo kwa tendo Lake, kwamba mtakatifu aliye dhaifu kuliko wote duniani anaweza kumshinda ibilisi juu ya Neno la Mungu lililoandikwa. Yeye alikuwa ni Mungu Mwenyewe, aliyedhihirishwa katika mwili, alikuwa na nguvu zisizo na kikomo, bali kamwe hakuzitumia. Yeye alifanya nini?

Alimshinda Shetani juu ya Kitu kile kile ambacho Shetani alimshindia Hawa. Amina. Wakati huyo yeye alimpumbaza.

126 Wakati alipopaka Neno la Mungu chokaa kwa Hawa, naye akaliamini, lakini alipokuja kujaribu kulipaka chokaa kwa Yesu, alishindwa. Naam, bwana. Alishindwa kwa sababu Yeye alidumu na Neno la Baba, kasema, "Imeandikwa, msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu Yeye peke yake."

127 Alifanya nini? Shetani alisema aliachana naye, maana alilichukua Neno la Mungu, halikuwa chotara Kwake. Yeye alikuwa Mwana wa Mungu aliye hai, asiyeghoshiwa, aliyezaliwa na bikira. Yeye hakuwa akimpaka chokaa, akilipaka chokaa Neno, hakuwa akimchanganyishia mbegu. La hasha, Yeye alikuwa amezaliwa na Mungu. Alitoka kwa Mungu, akaenda kwa Mungu, alidumu kwenye Neno la Mungu, kamwe hakutofautiana Nalo hata kidogo. Alipokuja, Yeye alifanya ishara za Masihi ambazo Biblia ilisema angefanya, nalo lile kanisa chotara lisiloamini katika siku hiyo halikuamini jambo hilo. Na wakati anapofanya jambo hilo siku hizi, wangali hawaliamini, kwa sababu ni chotara.

128 Kasema, "Haikuwa hivyo tangu mwanzo." Alipokuja, aliona watu wakifundisha mambo ambayo hayakuwa katika Biblia, na ndipo Yeye akasema, "Haikuwa hivyo tangu mwanzo." Sijui kama Yeye akija leo, angekuta wengi wao wakifundisha mambo ambayo hayakuwa katika Biblia, angesema jambo lile lile, "Haikuwa hivyo tangu mwanzo." Ni kweli.

129 Sasa, tunaona mambo aliyoyakuta, wakati alipokuja akaona kanisa. . .Sikilizeni, na hebu hili lizame vizuri na kwenye kilindi. Alipokuja, alikuta nini? Aliwakuta watu wakilitazamia kanisa kwa ajili ya wokovu. Nao walikuwa wakipata nini? Lundo la kanuni za imani. Na kwamba jambo lilo hilo lipo leo, lundo la kanuni za imani za kujibunia.

130 Wokovu huja kupitia Damu na hiyo pekee. Na kama una wokovu, Yesu Kristo alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Na kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Huo ni wokovu, huo ndio ushahidi wake, itakuwa vivyo hivyo.

131 Huko katika nchi za makafiri, wanaume kwa wanawake, nimewaona wakija kule ambao hata hawakujua ni upi mkono wa kulia na wa kushoto, kisha wakimpokea Roho Mtakatifu, mnajua wanafanya nini? Jambo lile lile mnalofanya, kunena kwa lugha, kumsifu Mungu, kuruka juu chini, wanaendelea tu kama mnavyofanya. Inaonyesha ya kwamba ni Mungu.

132 Nami nawatakeni ninyi wanawake wa Marekani mruhusu jambo hili lizame ndani yenu: Inawabidi kuvaa maskini nguo hizi chafu ili kutoka na kukata nyasi uani wakati wanaume wanapotoka kazini, mnawaacha binti zenu wafanye jambo lile lile. Sasa, nina wasichana wawili, huenda wakafanya hivyo wakati fulani, lakini, ndugu, watakapofanya hivyo, kujinyoosha

ukingoni mahali fulani, kasema kusudi wapate mbabuko wa jua, watapata mbabuko wa mwana, itakuwa ni mwana wa Bw. Charlie Branham na kiboko mkononi mwake. Watatiwa mbabuko kweli, hapana shaka juu ya hilo. Huyo atakuwa ni mwana wa baba yangu anayefanya hivyo. Mnaona? Lakini sasa, kwa—kwamba siku hizi...Nao...Tunadhaniwa kuwa wastaarabu.

133 Nilimwona mama mmoja akija hivi majuzi, huko chini kwenye Mkahawa huu wa Cliftons...Gene, tulikuwa huko juu. Ndugu Arganbright alikuwa akitaka kuninunulia suti, nami nilikuwa nikimngojea kwa sababu nilihitaji moja. Na—naye alikuwa akitaka kuninunulia suti, basi nilikuwa nikingojea kule Cliftons, nami nilikuwa nikimngojea aingie, nami nikaona mwa—mwanamke akiingia ndipo nikasema, "Jamani, maskini kitu hicho!" Nikamtazama, nikawazia...Mwajua, ni—ni—nilikuwa nimeona glakoma, nilikuwa nimeona ofthalmia, nilikuwa nimeuona ukoma, lakini si—sijawahi kuona kitu kama hicho, macho ya mwanamke huyo yalikuwa na kasoro. Ndipo nikawazia, "Vema, ninaamini nitaenda pale na kumwuliza dada huyo, nimwambie ya kwamba mimi ni mhudumu, na—na kumwuliza ana shida gani, na kama ningeweza kumwombea."

134 Na kwa hiyo nikaelekea kule, ndipo akatokea mwanamke mwingine aliyefanana naye, nikarudi nyuma. Labda angenipiga kofi kama ningemwuliza. Lakini mwajua, alikuwa amepaka macho yake rangi ya kijani kibichi *hapa* nje, bluu *hapa* nyuma, mwonekano wa kuchukiza sana niliowahi kuona maishani mwangu.

135 Sasa, enyi wanawake, basi kama mtavaa takataka hiyo, ambayo hampaswi kuivaa, hampaswi kuivaa, lakini mbona msijaribu kuonekana kama binadamu angalau? Si kama kitu fulani kilichoanguka kutoka kwenye, maiti, kutoka kwenye kituo cha mazishi, ama kitu fulani. Mimi—mimi...Angalau jaribu kuwa binadamu nayo.

136 Nami siamini katika kujipaka rangi hata kidogo, siamini mnapaswa kujipaka rangi. Kulikuwa na mwanamke mmoja tu katika Biblia aliyewahi kujipaka rangi usoni apate kukutana na mwanamume, (Hakuna mwanamke anayeupaka rangi uso wake akakutane na Mungu, unaupaka rangi uso wako upate kukutana na wanaume.), nalo jina lake lilikuwa Yezebeli. Unajua kile Mungu alichomfanyia? Alimlisha kwa mbwa. Kwa hiyo unapowaona wanawake wamejipaka rangi, basi unajua huyo ni Binti Nyama ya Mbwa, Mungu humpa mbwa, hilo tu ndilo linalomfaa ni nyama ya mbwa.

137 Ilikuwa kwamba wanawake wa Kipentekoste hawakufanya hivyo, bali sijui kilichotukia. Ilikuwa ni kosa kwa wanawake wa Kipentekoste kukata nywele zao. Hiyo ni kweli. Biblia inasema mwanamke yeyote anayekata nywele zake, mumewe ana haki ya

kumwacha, kumpa talaka, kwa sababu yeye ni mwanamke asiye na heshima. Biblia ilisema ya kwamba, loo, hakika Yeye alifanya hivyo, bila shaka alifanya hivyo. Loo, nini sasa? Haya basi.

138 Tunachohitaji ni Injili kutoka mimbarani, "Jinyoosheni," kote kote kutoka mimbarani hadi kwa bawabu. Hiyo ni kweli. Tunahitaji uamsho wa mtindo wa kale, wa Mtakatifu Paulo na Roho Mtakatifu wa Biblia. Mungu habadiliki hata kidogo. Yeye ni . . . Huo ulikuwa ndio uamuzi Wake, alitaka wanaume waonekane tofauti na wanawake, wanawake na wanaume, wavae tofauti, na hivyo ndivyo alivyowaumba. Tunapofanya jambo lolote kinyume na hilo, tunaenda kinyume na mapenzi ya Mungu, na sheria za Mungu, na mambo ya Mungu, wala hakuna cha kufanya ila kuyalipia, nasi tutayalipia, pia.

139 Tunawezaje kuwa na uamsho? Haidhuru kama kuna akina Oral Roberts, na Tommy Hicks, na Osborn kote nchini, mpaka tutakaporudi kwenye maisha halisi ya Kipentekoste, kamwe hatutaweza kujenga juu ya kitu chochote bado. Madhehebu yetu yanapata nguvu wakati wote, nasi tunapanuka wakati wote, pia tunakuwa wanatheolojia walioelimika vizuri zaidi wakati wote, lakini tunazidi kudhoofika, na kudhoofika, na kudhoofika wakati wote. Kweli kabisa. Rudini!

140 Mngekuwa afadhali kama mlikuwa na tari lenu, bila soksi, hapa chini pembeni mahali fulani, katika mkutano wa mtaani, kuliko vile mngekuwa katika baadhi ya hizo nyumba kubwa mno za maiti tunazopata, huku halijoto ndani yake ikiwa tisini chini ya sufuri, tukinena kiroho, kweli. Ni kweli kabisa. Tunahitaji Pentekoste! Ninapenda Pentekoste nzuri, ya mtindo wa kale, Roho halisi wa Mungu aliye hai. Ni kweli.

141 Sasa, katika siku Zake aliwaona watu wakifundisha mambo yaliyokuwa hivyo. Tuna jambo lile lile leo, halafu watu wote, baada ya kumaliza mambo haya yote, (Naye Yesu alisema, "Kwa mapokeo yenu mmezitangua amri za Mungu. Amri za Mungu zilisema, 'Utafanya *hivi*,' nawe unasema 'Utafanya *hivi*.'" Yeye alifanya nini? Lilikuwa ni jambo lile lile, walikuwa wamezipotosha amri za Mungu, hilo ndilo jambo lile lile Yeye angesema leo.), halafu watu wanasema, "Yuko wapi yule Mungu wa Biblia?" Huh!

Nilikuwa nikishirikiana na maskini mhubiri wa Kimethodisti, alikuwa akiimba wimbo:

> Tulilegeza kamba, tulilegeza kamba,
> Tulipatana na dhambi.
> Tulilegeza kamba, kondoo wakatoka nje,
> Lakini mbuzi waliingiaje?

142 Nakwambia ndugu, hebu jibu hilo, unapoimba huo wimbo: Mlilegeza kamba! Hiyo ndiyo shida. Hiyo ndiyo shida yetu sisi Wapentekoste. Hilo ni jambo moja kulihusu, sina mikutano yoyote mikubwa ya kudhamini, si lazima niwe na pesa nyingi,

hakuna mtu anayenikodi, hakuna mtu anayenilipa, kwa hiyo ninaweza tu kuhubiri yaliyo katika Biblia. Kweli. Hakuna mtu anayeweza kuniambia la kufanya. Naam, bwana.

> Tulilegeza kamba,
> Tukapatana na dhambi.
> Kulegeza kamba, kondoo wakatoka nje,
> Lakini mbuzi waliingiaje?

143 Legeza tu kamba, wataingia, kwa vyovyote vile. Unaona? Hiyo ni kweli. Loo, tunaninii . . . Tulikuwa tukisema, “Maskini Wamethodisti baridi wa kawaida,” na sasa Wamethodisti wanasema, “Maskini Wapentekoste baridi wa kawaida.” Hiyo ni kweli. Inakuwa vivyo hivyo. Loo, aibu kwetu! Tunachohitaji ni uamsho. Uamsho haumaanishi kuleta wafuasi wapya, ni kuamsha kile tulicho nacho tayari. Kweli.

144 Nilisimama karibu na Ziwa Michigan kwa mara yangu ya kwanza miaka mingi iliyopita, yapata miaka thelathini iliyopita, nilienda kumsikiliza Paul Rader, rafiki yangu, akihubiri ibada ya mapambazuko kwenye ibada ya Pasaka, ibada ya mapambazuko. Nikatembea huku na huko kwenye Ziwa hilo la Michigan, lilikuwa ndilo eneo kubwa zaidi la maji . . . lilionekana kubwa sana kuliko Mto Ohio kwangu mimi. Nami nikaliangalia, na, loo, jamani, yalikuwa tu yakiruka na kuruka, hayo mawimbi, nikawaza, “Kwa nini unarukaruka hivi? Una shida gani?”

145 Nikaendelea kutembea ufukoni mwa hilo ziwa asubuhi hiyo baada ya ibada, nami nikawaza, “Unarukia nini?” Nikasimama, nami nikawazia, “Vema, ha—ha—hakuna sababu ya wewe kuruka, nionavyo mimi.” Nami nikawaza, “Vema, labda una maji mengi ndani yake.”

Likasema, “La.”

146 Nikawazia, “Halina maji mengi zaidi ndani yake, kuliko wakati limetulia kabisa, halina tone moja zaidi la maji.” Wakati yanaporuka, mawimbi yakipiga, ni kiasi kile kile cha maji, hamna tone moja zaidi ndani yake.

147 Vema, nikawaza basi, “Vema, una—unarukia nini basi?” Nami nikawazia, “Vema, lina uamsho. Hivyo ndivyo ilivyo, lina uamsho.” Vema, kama halikuwa na uamsho, lingejaa takataka. Lakini kila wakati upepo unapolipiga, na kuanza kuvuma, linaruka na kuendelea, na kufagilia mbali uchafu wote ukingoni, maskini vijiti vyote, na uchafu ukingoni.

148 Na huo ndio ninii, sisi, Kanisa linahitaji, linahitaji uamsho. Basi ni kitu gani kinachoanzisha upepo huu? Ni kitu gani kinachoanzisha huu unaoendelea, uamsho huu? Unakuja upepo, “*whiu*,” unaokota *vyote*. Huo ndio tunaohitaji ni Upepo mwingine Mkuu unaoenda Kasi kuanzisha uamsho, kuondoa takataka za Kanisa, na kutokuamini. Kuondoa kutokuamini kwetu *kwote*, kukulundika ukingoni, na tufanye mkutano halisi

wa Kipentekoste, mkutano halisi, wa kweli. Amina. Huo ndio tunaohitaji. Ndivyo hasa. Shh!

[Dada mmoja ananena kwa lugha kisha ndugu fulani anafasiri—Mh.]

149 Amina. Sasa, kwamba kunaweza kuwa na wengine ambao hawataelewa hilo, hizo ni karama za kimitume. Wakati . . . Ili kuwatulizia tu hili kwa dakika moja, hebu niwakumbushe tu jambo fulani papa hapa, dakika moja tu.

150 Hivi majuzi kwenye Wafanyabiashara Wakristo huko Los Angeles, nilikuwa nikihubiri kwenye kiamshakinywa chao, ambacho kilitangazwa kote nchini, nilikuwa nikirarua kitu hicho kwa nguvu nilivyoweza. Siwezi kufanya lingine lolote, kama ningefanya hivyo, ningekuwa mnafiki, ninaamini tuko katika wakati wa mwisho. Basi nilipofanya hivyo, Marilyn Monroe, binamu yake, Mbaptisti, alikuja kunisalimia kwa mkono, na alipofanya hivyo, alianza kunena kwa lugha. Basi alipofanya hivyo, yeye . . .

151 Kulikuwa na mama kutoka Louisiana ameketi huko nje, mwanamke Mfaransa, akasimama, na kusema, "Hizo si lugha zisizojulikana," kasema, "Mimi ni Mfaransa. *Haya* ndiyo aliyosema."

152 Kisha mtu mwingine alikuwa amekuja hapa. Na huko chini kupitia pale jamaa mdogo akanyemelea, akishuka, ambaye alikuwa mfasiri wa Kifaransa wa UN, Umoja wa Mataifa, ndio kwanza apeperuke mkutanoni, naye akasema, "Haya *hapa* aliyosema," jambo lile lile kabisa.

153 Naye mvulana huyu, binamu wa Marilyn Monroe, Danny Henry, hakujua hata neno moja la Kifaransa. Naye . . . Ninayo papa hapa, ambayo yataandikwa, wengi wenu mtayaona katika lile la *Wafanyabiashara*. Sasa, hili hapa jambo hasa, yale aliyosema, akiniambia, loo, ilisema, "Ilinenwa kwa Ndugu Branham tarehe 11 Februari, katika—katika mwaka wa 1961, kwenye kiamshakinywa cha Wafanyabiashara wa Full Gospel."

> *Kwa sababu umechagua njia nyembamba, njia iliyo ngumu zaidi, umetembea kwa hiari yako mwenyewe, . . .*

Ninaweza kuelewa hilo. Musa alitembea kwa hiari yake mwenyewe pia, haikumbidi kufanya hivyo. Ningeweza labda kuwa na mikutano mikubwa, mambo makubwa, na madoido mengi sana, makubwa, na kadhalika, pia. Lakini hii ndiyo njia nimetamani. Mnaona?

> *. . . umetembea kwa hiari yako mwenyewe, umechagua uamuzi sahihi na dhahiri, na hii ni NJIA YANGU.*
>
> *Kwa sababu ya uamuzi huu muhimu sana, sehemu kubwa ya Mbinguni inakungojea.*

Hayo yamo katika ono hapa, ambalo mtapata, mnaona, kwamba hakujua lolote kulihusu wakati huo.

*Ni uamuzi mtukufu jinsi gani uliofanya!*

*Hili*. . .(Sasa, haya ndiyo sielewi.) *Hili ndilo litakaloleta, na kutimiza, ule ushindi mkuu katika Upendo wa Kiungu.*

154 Pamoja na wakalimani watatu mbalimbali, wakalimani wa Kifaransa, na mkalimani wa Umoja wa Mataifa! Na Danny Henry, Marilyn, ama, ilikuwa ni huyu Jane Russell, samahani, binamu ya Jane Russell, Mbaptisti, hakujua hata neno moja lake, bali alikuwa mkali sana, alipanda juu na kusema, "Ndugu Branham, hayo maneno uliyosema yangeweza kuwekwa katika Kitabu cha Ufunuo kwa urahisi." Akanikumbatia, akaanza kuzungumza Kifaransa, kamwe hakujua hata neno moja lake. Kuna mashahidi watatu wanaoshuhudia, pamoja na mkalimani wa Umoja wa Mataifa. Ndugu, tuko katika siku za mwisho, hiyo ni kweli kabisa. Amina.

155 Niko mbali. . .Ondokeni kwenye dini chotara, ingieni kwenye Upentekoste wa kweli, halisi. Hiyo ni kweli.

156 Wanasema leo kama walivyosema wakati huo. Yesu alikutana na watu waliofundisha mambo ambayo hayakuwa ya kweli. Kanisa la kwanza lilifanya nini? Ninataka kumwuliza mtu hapa ambaye huenda akawa, haelewi hili. Kanisa la kwanza, walifanya hivyo. Sasa, kama ilivyokuwa wakati huo, ndivyo ilivyo sasa.

157 Inanikumbusha, siku hizi, juu ya Yesu wakati mmoja, na mama Yake, katika kufunga, sikilizeni, mama na baba Yake, walienda mpaka, ama, baba Yake mlezi, hadi kwenye sikukuu ya Pentekoste, ambayo ilikuwa ni desturi yao kupanda kule kila mwaka kwenye Sikukuu ya Pentekoste, na baada ya hiyo sikukuu kwisha, wakaanza kwenda nyumbani, nao wakaenda safari ya siku tatu, na kumkosa, safari ya siku tatu. Loo, wakiwazia tu, labda, "Yeye yuko miongoni mwa hilo kundi."

158 Sikilizeni, sitaki kuudhi hisia zenu, lakini hivyo ndivyo kanisa limefanya, kuwazia tu, labda, "Yeye yuko pamoja nasi, kwa hiyo inaleta tofauti gani? Loo, Yeye, Yeye yuko pamoja nasi." Lakini walifanya nini? Walirudi na kumtafuta kwa hizo siku tatu miongoni mwa jamaa zao, wala hawakumwona.

159 Na sasa hapa tuko kwenye wakati wa mwisho, wakati Billy Graham, mwinjilisti mashuhuri; Jack Shuler, Wamethodisti, rafiki msiri wangu; mzee Dk. Barr, hao, watu mashuhuri wamelitikisa hili taifa kwa uamsho. Nao uko wapi? Tunakunywa wiski nyingi zaidi kila mwaka, kuliko tulivyokunywa mwaka uliotangulia.

160 Ninaweza kuwaambia, hebu kila mnywaji wiski na mvuta sigara waweke chini sigara zao, na tumbaku, na wiski kwa siku moja kote Marekani, na kukusanya pesa hizo, zitampa kila mtu nyumba ya vyumba vitano, huyo ni maskini, na motokaa. Nyingi zaidi zilitumiwa mwaka jana kwa wiski kuliko zilizotumiwa kwa chakula. Basi vipi kuhusu Coca-Cola, kutafuna chingamu,

na anasa zingine tunazoishi ndani yake? Loo, tunaninii... Hamwelewi. Ni hali ya jinsi gani!

161 Lakini hapa, "Tulifikiri tu Kristo alikuwa pamoja nasi." Tumefanya nini? Sasa katika siku za mwisho, wakati mambo haya yamejitokeza, tunaanza kushangaa, "Yuko wapi? Yuko wapi?" Tumetafuta katika uamsho wa Kibatisti, hatumwoni kama alivyokuwa huko nyuma. Tunaangalia kupitia kwa Methodisti, hatumwoni; tunarudi siku nyingine, kwa ya Kilutheri, hatumwoni; tunarudi kwa Katoliki, hatumwoni.

162 Tulimpotezea wapi? Mahali Mariamu na Yusufu walipomkuta, hapo ndipo tutakapompata. Walimwacha kwenye Sikukuu ya Pentekoste, hapo ndipo tutakapompata tena, huko nyuma kwenye Sikukuu ya Pentekoste. Haleluya! Utukufu!

163 Huenda mkafikiri mimi nina kichaa. Labda ninacho, kama ninacho, achaneni nami, ninajisikia vizuri zaidi hivi, nina hakikisho zaidi namna hii. Naam.

164 Walimwacha wapi? Kwenye Sikukuu ya Pentekoste. Kanisa lilimwacha Kristo wapi? Huko Pentekoste. Ndipo likaja kanisa Katoliki; ndipo likaja kanisa la Kilutheri, madhehebu yote; ndipo likaja kanisa la Kiwesley, madhehebu yote; kanisa la Kibatisti, madhehebu yote; nao Wapentekoste wamefanya jambo lile lile. Tunafanya nini? Kuliweka kwenye rafu, kama tu hao wengine walivyofanya.

165 Hebu tuamke na kujitikisa. Hebu turudi kwenye sikukuu ya Pentekoste, na tuuondokee mpango huu wote wa elimu. Sijaribu kuunga mkono ujinga wangu, bali ninajaribu kuwaambia Neno la Mungu. Petro asingeweza kuandika jina lake mwenyewe, bali ilimpendeza Yesu kumpa funguo za Ufalme kwa sababu ya ufunuo wake. Hiyo ni kweli, ndugu zangu. Hiyo ni kweli.

166 Walimpata wapi? Huko nyuma kwenye sikukuu ya Pentekoste. Na huko ndiko ninyi Wamethodisti mtakakompata, huko ndiko ninyi Wabaptisti mtakakompata, huko ndiko ninyi Walutheri mtakakompata, huko ndiko ninyi Wakatoliki mtakakompata, kamwe hutampata miongoni mwa makanisa ya kwenu.

167 Ninyi watu wote mnaohamisha barua yenu kutoka kwa Methodisti, mkaipeleka kwa Baptisti, Yeye hatakuwa huko; mnaihamisha kutoka kwa Baptisti, nanyi nyote mnarudi kwa Katoliki, kamwe hamtampata huko. Rudini mahali kanisa lilipomwacha, kwenye Sikukuu ya Pentekoste wakati Roho Mtakatifu alipokuja kutoka Mbinguni kama upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote walimokuwa wameketi, Ndimi zilizogawanyika zikakaa juu yao, kama moto. Hapo ndipo mtakapomkosa, hapo ndipo mlipomwacha, hapo ndipo hatuna budi kurudi na kumchukua.

168 Sikilizeni, katika kufunga, Yesu alisema, "Mimi ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi." Na ni nini huo Mzabibu...? Huo

Mzabibu hauzai tunda lolote, tawi katika Mzabibu huzaa tunda. Uliwahi kuona mzabibu ukizaa zabibu? La, uliona matawi katika huo mzabibu yakizaa zabibu.

169 Vema, sasa hebu—hebu tuhoji jambo fulani. Ikiwa Mzabibu huo, ambao ni Kristo, Yohana Mtakatifu mlango wa 15 (Mnaamini hilo, sivyo?), vema, kama Mzabibu huo wa kwanza ulileta M—Mzabibu wa kwanza ulileta tawi nalo lilikuwa ni tawi la Kipentekoste, kisha nyuma ya tawi hili wakaandika Kitabu cha Matendo (Hiyo ni kweli, ndugu?), kama Mzabibu huo ukipata kuchipusha tawi lingine, litakuwa ni tawi la Kipentekoste ambalo litaandika Kitabu cha Matendo nyuma yake.

170 Loo, unasema, "Lakini mimi ni *Fulani-wa-fulani*. Mimi ni wa . . . "

Haikuwa hivyo hapo mwanzo.

Kama ungesema, "Lakini, Yesu, unajua, mimi ni mfuasi wa ninii takatifu . . . "

Haikuwa hivyo hapo mwanzo. Hiyo ni kweli. Angesema jambo lile lile.

"Mbona, tunaamini ya kwamba siku za miujiza zimepita."

Haikuwa hivyo hapo mwanzo.

"Hatuamini inakubidi kunena kwa lugha."

Haikuwa hivyo hapo mwanzo.

"Hatuamini katika uponyaji wa Kiungu."

171 Haikuwa hivyo hapo mwanzo. Rudini kwenye mwanzo, rudini mahali Kanisa lilipoanzia, Nalo lilianza kwenye Siku ya Pentekoste, huku Roho Mtakatifu akimiminika juu ya watu, na kuijaza mioyo yao, na kuzichangamsha nafsi zao mpaka wakafa kama wafia imani, wakaiteketeza dunia kwa ujumbe wao wa wokovu. Ondokeni kwenye kanuni zetu za imani za kujibunia, na mrudi kwenye Biblia. Naam, rudini hapo mwanzo, hapo ndipo tunapoanzia.

172 Sasa, angalieni, nilisimama . . . Sasa, sote tunajua, kusudi niwafafanulie hili, sisi ni Mti uliopandikizwa, hiyo ni kweli, bali tumepandikizwa katika Yesu Kristo kutoka kwenye ile othodoksi ya kale ya Kiyahudi mpaka Mti wote sasa ni Yesu, tumepandikizwa kwa huo.

173 Lakini hebu niwaonyeshe jambo fulani, nilikuwa Phoenix hivi majuzi ambako niliona matunda kadhaa yakikua kwenye mchungwa mmoja. Kulikuwa na limau, na balungi, na chenza, na kila namna ya matunda yakikua kutoka kwenye—kutoka kwenye mchungwa. Nami nikamwambia Ndugu John Sharrit, ndugu Mpentekoste, nikasema, "Ndugu John, nini . . . ? Kwani huo—huo si—huo si ni . . . ? Ungeuita mti wa—wa aina gani huo?"

Naye akasema, "Huo ni mchungwa."

174 Vema, nikasema, "Unakuwaje na malimau juu yake, na unakuwaje na balungi, na makangaja, na machenza, na, loo, aina mbalimbali za matunda jamii ya mchungwa?"

"Loo," akasema, "yalipandikizwa kwake."

Nikasema, "Lakini nataka kukuuliza jambo fulani. Sasa, wakati wa kuchanua utakapowadia, je, huo mbalungi utachanua?"

"Naam, bwana."

"Je, mlimau huchanua?"

"Naam, bwana, papa hapa kwenye mchungwa."

175 "Lakini unazaa tunda la aina gani maana unaishi katika mti huu? Je, unazaa matunda ya namna ile ile ambayo . . .? Je, huo, mwaka ujao, utazaa machungwa?"

Akasema, "La, bwana."

"Kwani utazaa nini?"

Akasema, "Balungi. Mlimau utazaa malimau."

Nikasema, "Huku ukiishi kwenye mti huu?"

Akasema, "Naam."

Nikasema, "Haleluya! Ninaliona sasa."

176 Ndugu, Kanisa ni Kanisa la Kipentekoste. Uhai ulio katika ule Mzabibu huingia kwenye Kanisa moja na kulipa tukio la Kipentekoste, na nyuma Yake walikuwa na kila namna ya karama za Roho Mtakatifu, ishara za Yesu Kristo. Na siku hizi tumepandikiza kila namna ya madhehebu ndani Yake, Methodisti, Baptisti, Presbiteri, hata na Pentekoste, *wanavyojiita*, wamepandikizwa ndani Yake, bali hawazai tunda la asili, hawana lile tukio la asili, hata hivyo wananyonya kutoka kwenye jina la Ukristo. Haleluya! Hiyo ni kweli.

177 Mzabibu huo ukipata kuzaa tawi lingine, litakuwa ni tawi la Kipentekoste lenye ishara zinazomfuata mwaminio. Kweli. Rudini kwenye ya Asili, mambo haya chotara hayatafaa kitu. Ninajua wamejibandika mle ndani, unaoitwa *Ukristo*, bali wao si Ukristo. Matunda, "Kwa matunda yao mtawatambua." Na kwa nini hawawezi? Kamwe hawawezi kurudi, kamwe hawawezi kuwa chungwa, kwa sababu wao ni chotara, hata hivyo, wanaenda chini ya jina la *Mkristo*, bali wao ni chotara. Utukufu!

178 Ninajua ya kwamba huenda mkafikiri nimerukwa na akili, lakini huo ndio ukweli. Kila wakati huo unapozaa, utafanya nini, kuwa na uamsho? Hakika, utazaa nini? Malimau. Mmethodisti atazaa Mmethodisti, Mbaptisti atazaa dhehebu la Kibaptisti, dhehebu la Kipentekoste litazaa Mpentekoste. Lakini watakaporudi kwenye ule Mzabibu asili uliotoka kwenye Shina, haleluya, watatokea na ubatizo wa Roho Mtakatifu, kama walivyofanya hapo mwanzo. Na kazi zile zile na

ishara zilizomfuata Yesu zitafuata, zilizolifuata Kanisa hilo la mwanzoni, zitalifuata Kanisa leo.

Unasema, "Mimi hufanya *hivi-na-vile*." Lakini haikuwa hivyo hapo mwanzo.

179 Ee Mungu, uurehemu udhaifu wetu, hali isiyokamilika, ni jambo la kusikitisha. Loo, jinsi . . . Watu wanamwogopa Roho Mtakatifu, unahofia itakufanya ufanye kitu ambacho—ambacho huenda ukafanya yasiyofaa, hatafanya hivyo. Watu wanaogopa.

180 Ninakumbuka nikisoma vitabu juu ya Pentekoste, miaka mingi iliyopita, wakati walipokuwa wakikaa usiku kucha madhabahuni na kuomba kwa siku kadhaa, Mungu angewaua chini ya nguvu za Mungu.

181 Na kwenu Wamethodisti, huko nyuma katika siku za kale, nena kuhusu uponyaji wa Kiungu, mnapaswa kujionea aibu kukana uponyaji wa Kiungu, wakati John Wesley, katika maelezo yake mwenyewe, kitabu chake mwenyewe, alipoandika ya kwamba alikuwa amempanda farasi wake, farasi wake alianguka na kuvunjika mguu, akaamka na kumpaka huyo farasi mafuta, katika Jina la Bwana, akampanda akaenda zake. Kuna ni—ninii . . .

182 Na huko Uingereza inasemekana kwamba alikuwa akihubiri juu ya uponyaji wa Kiungu, nalo kanisa la Kianglikana lililokuwa likimdhihaki huyo mwanzilishi hasa wa Umethodisti, ndipo kanisa la Kianglikana likamwachilia mbweha, na kundi la mbwa wakali, miongoni mwao, naye John akaelekeza kidole chake usoni mwake, na kusema, "Jua halitatua juu ya kichwa chako mara tatu, mpaka utakaponiita nikuombee." Ndipo mtu huyo akafa alasiri hiyo akimwita John.

183 Nilipanda matandiko yake, ama, niliketi kwenye tandiko lake ambapo alikuwa ameweka maskini dawati lake nyuma, nikaketi ma—mahali pake ambapo alimwongoa yule mpiganaji wa jogoo wakati huo kwenye kiti hiki, niliwekelea joho lake begani mwangu, nikapiga magoti sakafuni huyo mtu mtauwa alipofia, na kuomba na kumshukuru Mungu kwa ajili ya mtu kama John Wesley. Angepinduka kaburini mwake usiku wa leo, akijua kanisa la Kimethodisti linakuwa baridi na kuyarudia mapokeo ya wanadamu, badala ya kudumu na Neno hilo.

184 Ninyi Wabaptisti, mnapaswa kupitia mkondo wa mavumbi ya mbao, pia. John Smith aliomba mpaka ninii yake, usiku kucha na kulia kwa ajili ya dhambi za watu, mpaka ilimbidi mke wake kumwongoza mezani asubuhi apate kumlisha, na kumlisha kwa kijiko.

185 Ninyi wanawake wa Kimethodisti mnaovaa kaptura, na kuvuta sigara, na kufanya yasiyofaa, maskini John Smith, Mmethodisti huyo mashuhuri, alipokuja, alihubiri mahubiri mafupi kwa muda wa saa nne, nanyi hamwezi kusikiliza dakika ishirini, wakati alipokuwa na umri wa miaka themanini. Naye

alisema, “Inahuzunisha moyo wangu kuona hata akina dada wa Methodisti wakivaa pete vidoleni mwao.” Vipi kuhusu kaptura sasa, na kuvuta sigara? Aibu kwenu!

186 Nanyi Wapentekoste mnazidi kuwa wabaya. Ondokeni kwake, msiwe mzabibu uliopandikizwa, rudini kwenye mwanzo wa asili na kumpokea Roho Mtakatifu kama walivyofanya kwenye Pentekoste. Amina. Usimwache askofu akushike, acha Kristo akushike. Nina furaha Mungu alinishika kabla kanisa halijanishika, ningekuwa kafiri.

187 Nina wasichana wawili wadogo nyumbani, mmoja wao anaitwa Sarah, na huyo mwingine anaitwa Rebekah. Rebekah kidogo ni msichana mwenye miguu mirefu, mnene, naye Sarah ni maskini jamaa mdogo, mfupi. Wote wawili ni wasichana wa baba, maana ninapenda watoto.

188 Nilikuwa nje mkutanoni, na nimechoka *sana*. Walikuwa, walingojea mpaka usiku wa manane, macho yao madogo yakawa mazito, ndipo ikawabidi kwenda kulala. Kwa hiyo nikaingia karibu saa saba, nami nilikuwa na usingizi sana nikajilaza chini, na kulala yapata saa moja ama mbili, nami nisingeweza kulala, ndipo nikaamka tu na kuketi kitini huko nje sebuleni.

189 Njia ndogo ya ukumbi huelekea kwenye chumba cha kulala cha watoto, mke wangu alikuwa bado amelala. Nilikuwa nimeketi hapo asubuhi hiyo, na baada ya kitambo kidogo nikasikia, kitu fulani kikienda mbio katika chumba cha kulala cha watoto, nikaangalia chini namna *hiyo*. Rebekah ndiye mkubwa, na kwa hiyo akaruka juu na kuangalia huku na huku akaona kumekucha. Na, loo, wote wawili wanampenda Baba. Nao hawa hapa...Rebekah akaja. Vema, hilo lilimwamsha Sarah.

190 Sasa, Bekah ana miguu mirefu kuliko wote naye ndiye mkubwa zaidi, kwa hiyo angeweza kumshinda Sarah mbio. Na kwa hiyo, ananikumbusha makanisa makubwa, yamekuwa dhehebu kwa muda mrefu, mwajua. Kwa hiyo akatoka mbio na kuitagaza miguu yake midogo kwenye yangu, akaitupa mikono yote miwili shingoni mwangu, akaanza kunikumbatia. Na, loo, mnajua jinsi hilo linavyonifanya nijisikie.

191 Ndipo muda si muda mwajua, huyu hapa maskini Sarah anakuja, dada, maskini mtoto mwenye macho meusi, yapata urefu *huu*, amevaa nguo za kuachiwa na Becky, sijui kama watoto wenu wanafanya hivyo au la, pajama zenye miguu ambazo, kubwa kupita kiasi. Naye huyu hapa anakuja, akianguka juu ya kila kitu alichopata, mlango.

192 Ndipo Rebekah akamtazama, akasema, “Sarah, dada yangu,” kasema, “Nataka ujue ya kwamba nilikuwa hapa kwanza,” kama tu baadhi ya makanisa makubwa, marefu ya kimadhehebu, mnaona, “Nilikuwa hapa kwanza, nami nina

Baba wote, wala hamna nafasi kwako hata kidogo." Hivyo ndivyo wanavyojaribu kulisema, bali halifanyi kazi vizuri.

193 Maskini mtoto Sarah akainamisha maskini kichwa chake, nami nikaona midomo yake midogo ikianza kutetemeka, machozi makubwa mno yakiingia machoni mwake. Nikamwangalia namna *hiyo* na kuashiria kidole changu, nikachomoza mguu huu mwingine nje. Huyu hapa anakuja.

194 Naye papo hapo akaurukia mguu huo. Naye alikuwa tu ni kanisa changa, mwajua, kitu kama hicho, alikuwa shaghalabaghala, asingeweza kushikilia vizuri sana, mwajua, hakujua theolojia zote na mambo unayopaswa kujua, mwajua, na haya yote kulihusu. Kwa hiyo, lakini hata hivyo, alikuwa ameketi mguuni pangu, ndipo nikamwona jamaa huyo mdogo aki—akitaka kuanguka, kwa hiyo nikanyosha mikono yote miwili na kumshika *hivi* na kumkumbatia.

195 Akaegemea kifuani mwangu kwa muda kidogo, naye akageuka, macho hayo makubwa ya hudhurungi yakamwangalia Rebekah, naye akasema, "Rebekah, dada yangu," naye akasema, "Nataka ujue jambo fulani, pia." Kisha kasema, "Huenda ikawa unaye Baba wote, ila nataka ujue, Baba ana mimi wote."

196 Hivyo ndivyo ninavyoamini, huenda nisijue the—theolojia yote ninayopaswa kujua, na huenda nisiwe nimekuwako muda mrefu sana, na ujuzi wa seminari wa muda mrefu, bali mradi tu ninajua Yeye amenikumbatia mimi wote mikononi Mwake, Naye anaweza kunitumia, hilo tu ndilo ninalojali kujua. Kusudi tu nijue kwamba Yeye ana mimi wote, hilo tu ndilo ninalojali. Kama Yeye ana mimi wote, basi hilo tu ndilo ninalojali. Si hilo ni kama tu vile unavyojisikia, pia? Mradi tu Yeye ana mimi wote!

Na tuinamishe vichwa vyetu.

197 Baba yetu wa Mbinguni, imeandikwa katika Maandiko, "Haikuwa hivyo tangu mwanzo." Kwa hiyo mimi, katika njia hii ndogo fidhuli ya kulileta, Bwana, Nimejaribu kupanda mbegu hapa katika mioyo ya watu hawa wapendwa, wa thamani, ambao ni Wakristo halisi, halisi sana, lakini ninajaribu kuwaelezea, Bwana, "Kamwe msijichanganyishe katika namna fulani ya jambo la kujibunia. Rudini kwenye mwanzo, rudini Pentekoste, hilo ndilo Kanisa la kwanza la Kikristo."

198 Kwenye Siku ya Pentekoste, lilizinduliwa, naye Petro akahubiri mahubiri ya kwanza, kasema, "Enyi watu wa Uyahudi, nanyi mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili, mkasikilize maneno yangu: Watu hawa hawajalewa kama mnavyodhania."

199 Ee Mungu, lileweshe Kanisa Lako kiroho mpaka watasahau mambo yote ya ulimwengu na shughuli za maisha, na kukupenda tu, na kukutumikia. Mioyo na isalimishwe mikononi Mwako,

Bwana. Tujalie. Waokoe waliopotea, warehemu wanaokufa, waponye wagonjwa.

200 Tunafundishwa katika Biblia ya kwamba Wewe ulipokuwa hapa duniani, uliwaonyesha ishara ya Masihi ulipoonyesha . . . ulipomwambia Petro yeye alikuwa ni nani; ulipomwambia yule mwanamke Msamaria, "Nenda, kamwite mumeo"; wakati yule mwanamke alipogusa vazi Lako, kisha akatoka na kuketi kwenye kusanyiko; wakati Wewe ulipojua ilikuwa ni Zakayo mtini; wakati Bartimayo kipofu, haiwezekani kwake kuisikia Sauti Yako, ama, Wewe kuisikia sauti yake huku vilio hivyo vyote vikiendelea, bali Yeye alikugusa, Nawe ukasimama; pia yule mwanamke aliyegusa vazi Lako, Wewe uligeuka, ukaangalia kwenye kusanyiko mpaka ukamwona, na kumwambia, "Imani yako imekuokoa."

201 Tunafundishwa, usiku wa leo, ya kwamba Wewe ni Kuhani Mkuu yeye yule anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, umeketi mkono wa kuume wa Mungu Baba, katika ukuu huko Juu, anayeishi daima akituombea tunapokiri. Mungu, tunakiri usiku wa leo, ya kwamba hatustahili baraka zozote, ama hatustahili kuitwa Wakristo, kwa sababu linatokana na neno *kuwa kama Kristo*. Tafadhali tusamehe njia zetu mbaya.

202 Nasi tunajua ya kwamba dhambi iliyo kuu kuliko zote, na dhambi pekee iliyopo, ni dhambi ya kutokuamini. Haidhuru tunaishi vizuri jinsi gani, jinsi tunavyohudhuria kanisa vizuri, jinsi tunavyohubiri Injili, kama hatuamini kila Neno la Neno la Mungu, na kulitekeleza vivyo hivyo, tungali ni wenye dhambi, ulisema hivyo, "Yeye asiyeamini amekwisha kuhukumiwa." Kwa hiyo ninakuomba Wewe, Baba, utupe imani.

203 Wabariki hawa wote, ndugu zangu wahudumu. Bariki kanisa hili, chuo hiki tulichomo, wako hapa wakiwaelimisha vijana wanaume wawe wahudumu wa kesho. Mungu, usiwaache watoke nje kama kundi la kuku wa kiangulio wasio na mama, wameanguliwa tu kimitambo, jalia waende na wokovu halisi. Jalia waondoke na tukio kama la John Wesley, kama la Dwight Moody, Knox, Calvin, Sankey, Finney, wale waanzilishi wa Kipentekoste. Tujalie, Bwana.

204 Tusamehe makosa yetu yote. Na kama tumekuchukiza kwa njia yoyote, jalia neema Yako na Damu Yako zifanye upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu. Waokoe waliopotea sasa, Baba, tunaomba, katika Jina la Yesu.

205 Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, macho yetu yamefumbwa, je, kuna mwenye dhambi humu jengoni angesema, "Ndugu Branham, nikumbuke sasa katika maombi, nimeketi hapa na kusikiliza, sitaki, tena, maungamo yoyote yaliyofanywa kwa mambo kichotara, kwa sababu ati nilijiunga na kanisa ambalo mama yangu alikuwa mfuasi wake; nilikuja shuleni kwa sababu mtu fulani alinishawishi kuja, mimi ni mwanafunzi

hapa shuleni, katika chuo hiki; mwanangu anahudhuria hapa; binti yangu anahudhuria hapa"?

206 Binti zangu wawili labda wataenda kwenye Chuo cha Asbury, huko Wilmore, Kentucky, ninaishi karibu na hapo. Ninawataka wawe Wakristo halisi. Mwanangu ndio kwanza atoke Waxahachie, ambako alisomea. Nasi tuko karibu na huko, tunaishi kule, ni karibu zaidi nasi, kwa hiyo tunaweza kuwaona hao wasichana. Tunataka wawe na yaliyo bora zaidi, tunataka kuwafanyia yote tuwezayo, lakini zaidi ya mambo yote, hata wakijua ABC zao, ninawataka wamjue Kristo, na wawe na tukio la kujazwa na Roho Mtakatifu.

207 Je, hivi huna Kristo usiku wa leo, na tukio la namna hiyo? Je, wewe ni mfuasi wa hali fulani ya kichotara? Wewe mwenyewe ni chotara, ukikiri kuwa Mkristo wakati hujawahi kumpokea Roho Mtakatifu? Kama ndivyo ulivyo, rafiki yangu mwenye fadhili na mpendwa sana, je, utainua mkono wako? Useme, "Nikumbuke katika maombi, Ndugu Branham. Sasa ninataka tukio halisi la Pentekoste moyoni mwangu. Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mbaptisti. Mimi ni mfuasi wa dhehebu la Kipentekoste, bali simjui Kristo kwa njia hiyo, kama walivyofanya kwenye Siku ya Pentekoste. Sina ujuzi waliokuwa nao hao watu. Nikumbuke, Ndugu Branham."

208 Vema, sioni mkono mmoja. Nami naami-. . .Mkono mmoja, Mungu akubariki, jamaa mdogo. Siamini ya kwamba mtu yeyote mwenye akili timamu, ya kawaida, ambaye angeweza kuketi hapa sasa, baada ya kusikia hayo yakielezewa namna hiyo, angeweza kutoka hapa na awe kama kawaida, isipokuwa umehukumiwa. Mnaona, kuna baadhi ya watu wasioweza kuja, Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja, asipovutwa na Baba Yangu. Wote alionipa Baba Yangu watakuja."

209 Hebu wazia tu jinsi ingekuwa kama ungalikuwa umetenda dhambi ukaimaliza siku yako ya neema, wala kamwe usingeweza tena. . .Unaweza kumkufuru Roho Mtakatifu, unajua, unene neno moja dhidi Yake, haidhuru ulilia ama kuomba kiasi gani, hutasamehewa hilo kamwe. Hivi hungechukia kuwa katika hali hiyo, hamna upendo moyoni mwako, ukijua ya kwamba kamwe hujapata kumpokea Kristo, hujawahi kuzaliwa kwa Roho, yule Roho Mtakatifu aliyekuja kwenye Siku ya Pentekoste?

210 Unasema, "Mimi ni mfuasi wa kanisa fulani." Ndugu, hiyo si zaidi ya kuwa wa chama fulani, ungeweza kuwa wa chama vivyo hivyo, na kuishi maisha mazuri, safi. Sipingi kujiunga na kanisa sasa, hilo ni sawa, ninii. . .kufikia sasa, ni sawa, lakini hilo silo ninalozungumzia usiku wa leo, ujumbe wangu ni, "Kurudi kwenye mwanzo." Na kama hujapata tukio hilo lililokufanya utende na kufanya kama walivyofanya hapo mwanzo, basi

tafadhali, ndugu yangu, dada, inua mikono yako kwa Kristo na useme, "Nikumbuke, Kristo, nipe tukio hilo."

Asante, bwana, Mungu akubariki. Asante, bwana, Mungu akubariki.

211 Roshani? Kushoto? Roshani upande wa kulia? Ninangojea wakati kila mtu akiomba. Ro-. . .? Vema, safu za katikati, mahali popote? Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki huko nyuma, bwana. Ninangojea kuona uamuzi wako utakuwa nini.

212 Baba yetu wa Mbinguni, nangojea, nikitoa nafasi ya kutosha ili kwamba, kwenye Siku kuu ya Hukumu, kama Paulo wa kale alivyosema, "Hakuna damu ya mtu yeyote juu yangu."

213 Sasa, nimetoa na kufanya kama ulivyoniagiza, nijuavyo mimi, nami nimewaambia watu hawa ukweli. Ninaomba sasa ya kwamba utawarehemu, na utawaokoa wale walioinua mikono yao. Na wakati wito unapotolewa kwao kuja jukwaani, jalia waje kwa upendo, na kwa utamu, na hapa waungame, waingie chumbani, na kujazwa na Roho Mtakatifu, usiku wa leo. Tujalie, Bwana. Ninawakabidhi Kwako, katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Amina.

214 Sasa, kwa utulivu, kwa utulivu sana sasa, kila mtu katika sauti yako mwenyewe, sauti yako mwenyewe unayoimba:

> Mwokozi, Mwokozi,

Sasa hebu tumwabudu Yeye.

> . . .ninii yangu nyenyekevu. . .
> Wakati kwa wengine Wewe. . .
> Usinipite.

215 Loo, Yeye si ni wa ajabu? Mnampenda? Yeye si ni mwema? Mwajua, kumekuwako na uchaji mwingi zaidi usiku wa leo kuliko kawaida. Baadhi ya watu wameamka na kutoka nje, natumaini hiyo ilikuwa ni kwa sababu iliwabidi kuwahi basi, kitu fulani. Mimi. . .

216 Ndiyo sababu ya mimi kutokuwa na ibada ya uponyaji, wala siwezi kuwa nayo wakati watu wanazunguka-zunguka, Roho Mtakatifu ni mwoga, mtu yeyote anajua hilo, Yeye angeondoka tu, kama alivyofanya katika Biblia. Nanyi mnapozunguka-zunguka, inaninii tu—inakatiza tu, kamwe hamwezi kufanya hivyo. Kamwe hataninii. . .Angeniacha tu, nami ningesimama tu pale.

Kuna mgonjwa yeyote hapa? Inua mkono wako.

217 Ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Kama tunaamini ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho. . .Unaamini hilo, ndugu? Unaamini ujumbe ambao nimehubiri usiku wa leo ni kweli? Unakubali hilo? Vema, hebu na tumwite Roho Mtakatifu mkuu.

218 Sasa, Biblia ilisema ya kwamba ishara ambayo Mataifa wangepewa. . .Sasa, ni wangapi wanaojua ya kwamba hiyo ishara iko hapa usiku wa leo, na kuona yale Biblia ilisema juu yake? Sasa, ni wangapi wanaojua ya kwamba uponyaji wa Kiungu ni kitu ambacho tayari kimepita? Yesu alikuponya pale Kalvari. Hiyo ni kweli? Yeye alikuokoa, bali huna budi kuwa na imani na kuamini. Hiyo ni kweli?

219 Ni wangapi watakaoomba, na wawe na imani na kuamini ya kwamba Mungu, ya kwamba karama hii ya Mungu, Ujumbe katika siku za mwisho. . .? Ambapo tunajua Biblia ilisema, "Mungu ameweka ndani ya Kanisa mitume," (Hiyo ni kweli? Hao ni wamishenari, *mitume* ni "mtu aliyetumwa," *mmishenari* ni "mtu aliyetumwa.") "mitume, manabii, waalimu, wachungaji, wainjilisti." Hiyo ni kweli? Mungu aliziweka, ni karama za Mungu alizoweka Kanisani.

220 Ndipo katika kila kundi la mahali hapo kuna karama tisa za kiroho, hizo ni kunena kwa lugha, kufasiri lugha, maarifa, hekima, kila namna ya karama, karama tisa mbalimbali za kiroho.

221 Sasa, mnaamini, siku hizi, ya kwamba tuna mitume, wamishenari waliotumwa na Mungu? Mnaamini? Mnajua, hiyo ndiyo amri ya jumla, "Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili." Huyo ni mtume.

222 Mnaamini tuna manabii? Kuna karama ya unabii, halafu kuna nabii. Ni wangapi wanaojua kuna tofauti katika jambo hilo? Hapo ndipo ninyi watu wa thamani wa Mvua ya Vuli mlipochanganyikiwa. Mnaona? Nabii anazaliwa akiwa nabii, sikuzote ana BWANA ASEMA HIVI, kamwe hakosei, karama ya unabii ingekuwa juu ya mtu mmoja, kisha mwingine, na inabidi upambanuliwe na wapambanuzi watatu, kisha uambiwe kanisa, kisha waone kama utatimia.

223 Yeremia alikuwa ni nabii, Mungu alisema, "Kabla hata hujaumbwa katika tumbo la mama yako, nalikujua, na kukutakasa uwe nabii, na kukuweka kwa mataifa." Hiyo ni kweli.

224 Miaka mia saba na kumi na miwili kabla Yohana hajazaliwa, alikuwa ni sauti ya mtu aliaye nyikani, kwa nabii Isaya.

225 Yesu, kutoka bustani ya Edeni. Mnaona? Hatuwezi kuwa. . . Karama na miito havina majuto.

226 Sasa, ni wangapi wanaoamini ya kwamba Yesu Kristo aliahidi ya kwamba "Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, nitakuwa katikati yao"? Ni wangapi wanaojua ya kwamba Yeye aliahidi hili: "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya"? Ni wangapi wanaojua ya kwamba Yeye ni. . . ya kwamba jinsi alivyojithibitisha Mwenyewe kuwa Masihi, kwa sababu alikuwa ni Nabii? Ni wangapi wanaojua hilo? Biblia ilisema hivyo, Musa alisema, "Bwana Mungu wako

atakuondokeshea Nabii." Nalo kanisa liliamini nini siku hiyo? Wao walisema Yeye alikuwa ni mpiga ramli, Beelzebuli.

227 Mtu yeyote anajua mpiga ramli ni wa ibilisi. Uchawi wowote wa giza wa namna hiyo ni wa ibilisi. Lakini ni . . . Kuna—kuna *shida* gani? Ni kitu kizuri, kilichopotoshwa. Dhambi ni nini? Ni haki, iliyopotoshwa. Uzinzi ni nini? Tendo la haki, lililopotoshwa. Ni nini—ni nini u—uongo? Ni kweli, iliyopotoshwa. Mnaona?

228 Udhalimu wote . . . Ibilisi hawezi kuumba chochote. Ninii . . . Ninataka mtu fulani anionyeshe Maandiko ambapo ibilisi anaweza kuponya, ama ambapo ibilisi anaweza kuumba. Kuna Muumba mmoja tu, naye Shetani hupotosha kile Mungu alichoumba. Uumbaji wote hutoka kwa Mungu, Shetani hupotosha uumbaji.

229 Sasa, wakati alipokuwa duniani, jinsi watu walivyojua Yeye alikuwa ni Masihi, kama vile Filipo, alipoenda akamwona Nathanaeli, na kumwambia yale Yeye aliyomwambia Petro, aliporudi, mbona, alikuja Mbele za Yesu, naye Yesu akasema, "Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!" Hiyo ni kweli?

Kasema, "Ulinijua lini, Rabi?"

Kasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona."

"Unafanya nini, Ndugu Branham?"

230 Ninajaribu kumfanya Roho kufikia mahali ambapo tutaona yale atakayofanya, sijui. Simwongozi, Yeye huniongoza. Siwezi kuwaambia jambo moja, ni Yeye. Mimi ni bubu tu kama *hii* ilivyo bila kitu cha kuzungumzia ndani yake.

231 Lakini ni wangapi wanajua hilo, jinsi, Yeye alivyosema, ilikuwa ni katika siku za Sodoma, wakati Mungu alipokuja kule katika mwili wa mwanadamu, akimwakilisha Mungu katika siku za mwisho kabla ya kuteketezwa kwa dunia, kama alivyofanya wakati huo, Yesu alirejea kwake kwamba angekuja tena katika mwili wa kibinadamu, na angefanya jambo lile lile?

232 Sasa, angalieni, sasa, Yeye kamwe hakufanya yale Billy Graham na hao wengine waliyofanya, yale Malaika walioshuka Sodoma, waliyapofusha macho yao kule chini, kuhubiri Injili hufanya hivyo, lakini bila miujiza. Lakini mwangalie Yule aliyekaa huko nje kwa Kanisa la Kipentekoste ambalo Ibrahimu aliwakilisha, Kundi lililoitwa litoke. Yeye aliwapa nini kama ishara ya mwisho? Alikuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema na kuita, "Ibrahimu," siku chache tu hapo kabla lilikuwa limebadilishwa kutoka Abramu likawa Ibrahimu, kutoka S-a-r-a-i likawa S-a-r-a, Sara, "yu wapi Sara, mkeo?" Mgeni.

Kasema, "Yuko hemani, nyuma Yako."

233 Akasema, “Nitakurudia mwakani majira kama haya.” Naye Sara akacheka moyoni mwake. Akasema, “Kwa nini Sara akacheka, akisema, ‘Mambo haya yanawezekanaje?’” Hiyo ni kweli? Yesu alisema hilo lingejirudia tena.

234 Mnakumbuka wakati Yesu alipokuwa hapa? Alifanya hivyo mbele ya, Wayahudi na Wasamaria pia, bali si Mataifa. Walikuwa wakimtazamia Masihi, Yeye alionyesha ishara ya Masihi. Sasa, Mataifa walikuwa na miaka elfu mbili ya theolojia, bali Yeye alisema, kama nabii alivyosema, jua likichomoza asubuhi, likitua jioni, “Itakuwa nuru wakati wa jioni.” Jua lile lile lingeangaza magharibi, lile lile lililoangaza mashariki.

235 Ninadai kwamba Yeye hajafa, Yeye yu hai. Nami ninasema ya kwamba Roho Wake yuko hapa. Nguzo ile ile ya Moto iliyowafuata wana wa Israeli, iliyomtia mafuta Yesu Kristo, ni Roho yeye yule katika jengo hili, usiku wa leo, BWANA ASEMA HIVI. Itafanya kazi?

236 Ninaamini Billy alisambaza kadi chache za maombi hivi majuzi usiku, hatutaziita, kamwe hatutagusa kadi za maombi, kusudi mwone si kadi za maombi.

237 Hebu nibadilishe somo langu kwa dakika moja. Kulikuwa na mwanamke aliyegusa upindo wa vazi Lake. Labda asingeweza kuingia kwenye mstari wa maombi, hakuwa na kadi yoyote ya maombi. Lakini aligusa upindo wa . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

238 . . . mama nusura azimie, baba yangu akiinama karibu na kitanda, maskini Mkatoliki aliyerudi nyuma, bila kujua la kufanya, wakanichukua hadi kwenye kanisa dogo la Kibaptisti kuwekwa wakfu.

239 Ndipo miaka michache iliyopita, wakati hayo maono yalipoendelea kutokea, Wewe ulikutana nami huko Green’s Mill kwa Nuru kuu, iliyoangaza, ambapo Malaika alitokea ndani Yake, na kusema kwamba nilizaliwa kwa sababu hii.

240 Bwana Mungu, kuna wanafunzi wa chuo walioketi hapa, kuna mashaka, kuna fadhaa, kuna watu wanaoshangaa, Baba, wasamehe hilo. Ni, hawajawahi kuona kitu kama hicho, hawatambui ndiyo saa tunayoishi. Lakini Wewe uliahidi ishara hii kabla tu ulimwengu haujaangamizwa kwa Moto. Tunaona kwa sayansi, ya kwamba bomu la atomiki lina jina la taifa letu juu yake, ni mapambazuko na machweo mengine machache tu ya jua, labda hamna mengine.

241 Lakini, Baba Mungu, kuhusu ujumbe huu ambao nimehubiri kutoka moyoni mwangu, Neno Lako na ahadi Yako, uthibitishe usiku wa leo, Bwana, na kumjalia mtu fulani huko nje awe na imani ya kutosha kukugusa, ninapojisalimisha Kwako, ili uweze kusema nami maneno yale yale, kama ulivyomwambia yule mwanamke aliyetokwa na damu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

242 . . . Yesu Kristo, kwamba Yeye amesimama si futi mbili kutoka mahali nilipo sasa, Nuru ile ile. Nami ninachukua kila roho humu ndani chini ya mamlaka ya Roho Mtakatifu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Sasa nyamazeni, msisogee, kwa sababu pepo hutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine, nasi tunajua hilo. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . na kutenda jambo lilo hilo. Kama hutakuja, basi usiseme neno baya dhidi Yake tangu sasa na kuendelea, maana utakuwa unamkufuru Roho Mtakatifu na kuipeleka nafsi yako matesoni bila rehema. Na tuombe, tuiname . . . [Sehemu tupu kwenye kanda.]

. . . papa hapa, akiniangalia. Mnaona . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

243 . . . ana kitu fulani puani mwake, karibu na jicho lake, ni uvimbe mdogo wa kitu fulani. Anakiogopa kwa sababu kinaendelea kuja na kwenda, kinaambuka. Yeye ni mhubiri wa Injili. Sijawahi kumwona maishani mwangu, wala simjui. Je, una kadi ya maombi, bwana? Huna yoyote? Je, mambo hayo ni ya kweli? Inua mkono wako kama ni kweli.

Basi, ninataka kuwaulizeni nyote jambo fulani. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

“ . . . Nina kansa.” Je, hao . . . ? Ningewezaje kumwambia kile alichokuwa akiombea, na kile . . . ? [Sehemu tupu kwenye kanda.]

244 Hapa, kijana mwanamke akiniangalia, aliyeketi papa hapa, akiniangalia, chini kabisa, kama mtu wa pili ndani, kwenye safu hii hapa, anaumwa na kichwa, kitu kama kipandauso. Isitoshe, wewe ni mhubiri mwanamke. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Ninatangaza umeponywa, katika Jina la Yesu Kristo, ambaye alimgusa Kuhani Mkuu.

245 Kuna mwanamke wa makamu aliyeketi huko nyuma kabisa, amevaa koti la samawati lenye mapambo meupe, amevaa kofia ya samawati, anaugua ugonjwa wa kibofu nyongo. Kama utaamini kwa moyo wako wote, mama, unaweza kupokea uponyaji wako. Simama kwa miguu yako. Kama sikujui, punga mikono yako. Kama mambo hayo ni kweli, yale yaliyosemwa na Roho, pungeni mikono yenu. Basi ninatangaza umeponywa, katika Jina la Yesu Kristo.

246 Vipi kuhusu sehemu hii? Huyu hapa maskini mwanamke mmoja ameketi hapa, akiniangalia, papa hapa nje, koti jekundu, Nuru juu yake, anaugua ugonjwa wa figo. Simama kwa miguu yako. Ulikuwa ukiomba, “Bwana, jalia aniite.” Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Kama hatufahamiani, punga mkono wako. Ninatangaza kwamba umeponywa, katika Jina la Yesu Kristo.

247 Masihi, Mwana wa Mungu, Yeye Ndiye anayesema hilo.

248 Sasa nataka kuwaulizeni ninyi watu jambo fulani, Wamethodisti, Wabaptisti, Wakatoliki, na Wapresbiteri, kama

hawa Wapentekoste wamekosea, wanaonena kwa lugha, na kadhalika, kwa nini Masihi anawakilishwa, akionyesha ishara ya kufufuka Kwake?

249 Ni wangapi watampokea kama Mwokozi binafsi, na wanataka kujazwa na Roho Wake? Njoni hapa madhabahuni sasa hivi, ninyi mlioinua mikono yenu, pandeni hapa juu. Ninyi msiomjua Yeye, wala hamna Uzima huu wa Milele, njoni sasa, tunaposimama kwa miguu yetu na kuimba. Njoni sasa hivi. ("Nampenda, nampenda kwani Yeye kwanza. . .") Je, unampenda? Je, unataka kulielezea?

Nampenda, nampenda

Njoo, kila nafsi, njoo.

Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Wote wasiomjua Yeye kama Mwokozi wenu, hawajampokea Roho Mtakatifu, kwa nini msije? Kitu gani zaidi . . .?

250 Kumbukeni, hebu niwaambieni, ROHO WA MUNGU ALIYE JUU YANGU ASEMA HIVI: Hii ndiyo ishara ya mwisho kwa Kanisa la Mataifa kabla ya Kunyakuliwa.

251 NENO LA MUNGU LASEMA HIVI, ROHO MTAKATIFU ANENAYE ASEMA HIVI, AIJUAYE SIRI YA MOYO, BWANA ASEMA HIVI: Mnapokea wito wenu wa mwisho.

252 Niiteni *mlokole* mkitaka na kumkufuru Roho Mtakatifu. Njoo sasa kama huko tayari kukutana na Yeye katika Unyakuo. Ninatoa changamoto, ninaomba, ninashawishi, ninasihi: Njoni sasa!

Nampenda, nampenda

253 Kwa nini usisimame, huku Uwepo Wake ukiwa karibu sana? Ninyi wanafunzi wote hapa kutoka chuo hiki msio na Roho Mtakatifu, njoni vijana wanaume, wasichana, shukeni mje hivi, hiyo ni sawa.

. . . wokovu
Mtini Kalvari.

Nampenda, na . . .

254 Njoni sasa, njoni. Huu ndio wito wa mwisho, huenda ukawa ndio wa mwisho utakaowahi kusikia maishani mwako, kesho usiku huenda umechelewa sana kwako.

. . . mimi

255 Washiriki vuguvugu wa kanisa, hivi hamtakuja? Usiamini chotara, haitafufuka katika ule ufufuo, haiwezi kurudi tena. Njoo, upate tukio halisi. Rudini kanisani mwenu, Methodisti, Baptisti, Presbiteri, popote mlipo, rudini kwake, bali njoni mzaliwe sasa, njoni, mumpokee Roho Mtakatifu halisi.

Na. . .

Huko juu kwenye roshani, tunangojea.

Nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

256 Sasa, enyi marafiki, msimkatae. Ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Hivi utawahi, maishani mwako mwote, kufikia mahali popote ambapo unaona Neno lisiloghoshiwa, huku Mungu akija moja kwa moja nyuma ya hilo Neno na kujithibitisha Mwenyewe ya kwamba Yeye yupo hapa? Sasa, kuna wengine wenu huko nje. Mungu yeye yule ambaye angeweza kuniambia shida yako, ninajua shida yako, kwa neema Yake, kwa ufunuo Wake. Wengi zaidi wanahitaji kusimama hapa. Mara nyingine tena nitaimba. Pia kumbukeni, kwenye ile Siku ya Hukumu nitakapokutana nanyi, damu yenu haiko juu yangu. Mnakaribishwa kuja.

Nampenda. . .

Usibahatishe.

Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
. . .Kalvari.

Shuka uje, mpenzi, namna hiyo.

Mtini. . .

257 Watoto wadogo wanakuja, wakilia, hawajaikokota mioyo yao kupitia kwenye maskini magazeti ya *Hadithi Ya Kweli*, na kadhalika, kwa nguvu sana, hawana sugu.

Njoo, kipenzi, simama tu papa hapa juu. Wafanyakazi wa kibinafsi watakuwa hapa, katika dakika moja tu.

258 Nami sitaki uondoke pamoja na wafanyakazi wa kibinafsi mpaka nitakapowaombea watu hawa, mimi mwenyewe. Ninataka kuwaombea, pamoja na hawa ndugu.

259 Rafiki, unaweza kuona? Moja ya mambo hayo yangalitukia Afrika, maelfu, mara maelfu wangemiminika madhabahuni.

260 Sasa, nitawaulizeni jambo fulani. Ninataka uinamishe kichwa chako, huko kwenye kusanyiko. Nami ninawaomba, katika Jina la Yesu Kristo, ambaye mnasimama Mbele Zake, kama hujampokea Roho Mtakatifu, ingawa hutakuja huku, huninii. . .Ninataka uwe mwaminifu hivyo kwangu, na kwa Mungu, naye Mungu atawafanya msadikishwe, hakika, kama hujampokea Roho Mtakatifu, inua mkono wako, wote ambao hawajampokea.

(Nawatakeni mwangalie. Mnaona? Sasa, hiyo inaonyesha kama upambanuzi ni wa kweli au la, mnaona. Upo. Mnaona? Ni ninii tu, labda hiyo siku imepita.)

Ninataka wafanyakazi wa kibinafsi waje na kusimama karibu sasa. Kama hao wengine wangetaka kuja huku, njoni.

> . . . Nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua . . .

Wengi wanakuja pamoja na wafanyakazi wa kibinafsi, hilo ni sawa.

> . . . wokovu
> Mtini Kalvari.

261 Liwazieni, enyi marafiki, katika siku ambazo mataifa hayajui la kufanya, taifa letu, na ulimwengu huu uko kwenye kipipa cha baruti, mnajua hilo, si kipipa cha baruti, bali bomu la atomiki, unaenda kwenye kanisa *hili*, unaenda kwenye kanisa *lile*, unalikimbilia, si Biblia ilisema katika siku za mwisho itakuja njaa ya kusikia Neno la kweli la Mungu, watu wangeenda kutoka mashariki, magharibi, kaskazini, na kusini wakitafuta Neno la kweli la Mungu? Na hapa usiku wa leo, kwa kulisikia kutoka katika Biblia, pamoja na Roho Mtakatifu yeye yule aliyeiandika Biblia hapa, akithibitisha ya kwamba Yeye ni Yesu aliye hai papa hapa pamoja nasi usiku wa leo, ungewezaje kumkataa?

262 Nami nataka kuwaambia ninyi mliokuja, Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja, asipovutwa na Baba Yangu." Sasa, huyo alikuwa ni Mungu Baba yetu akisimama kando yako aliyekuleta kwenye jukwaa hili. "Yeye atakayenikiri Mimi mbele za watu, huyo nitamkiri mbele za Baba Yangu, na Malaika watakatifu." Nitawaombea kabla hatujaenda chu—chumbani.

263 Baba yetu wa Mbinguni, watu hawa wapendwa, wa thamani, wanadamu wapatikanao na mauti, hunywa, huzipenda familia zao na wapendwa wao, kama mwanadamu mwingine yeyote wa kawaida, huenda wamefanya mambo makuu maishani mwao, huenda wamefanya maamuzi mengi, lakini kamwe hawakufanya mmoja kama tu waliofanya hivi punde, kuja na kujazwa na Roho Mtakatifu wa Mungu. Ninaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba kila mmoja wao atampokea Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye yuko hapa sasa. Naomba . . .

61-0411 Lakini Haikuwa Hivyo Tangu Mwanzo
Illinois Wesleyan University
Bloomington, Illinois Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org